# Nipashe

Jumatatu Oktoba 23, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581472
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**Polisi** kumwekea ulinzi mwanafunzi aliyenajisiwa na baba yake miaka 3

UKURASA 4



**SMZ** yabuni mbinu mpya kuvutia watalii misimu yote

UKURASA 17

**WHO** yatoa maagizo sita kwa Israel

UK. 19




UKURASA 11

# HATIMAYE



• **Serikali,** DP World watia saini mikataba uendeshaji bandari kwa miaka 30, ajira za wazawa, mgawanyo wa mapato... *Ukurasa 2 & 4*

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Plasduce Mbossa (kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TPA, Balozi Ernest Mangu (wa pili kushoto) wakitia saini mkataba wa upangishaji wa gati namba 4 mpaka 7 katika Bandari ya Dar es Salaam baina ya Kampuni ya DP World ya Dubai iliyowakilishwa na Mkurugenzi Mtendaji wake, Sultan Ahmed bin Sulayem kwenye hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino, Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Kilichombeba Makonda uteuzi CCM

UKURASA 3



**MICHEZO** **YANGA, AZAM NI VITA YA KILELENI LEO** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Hatimaye mikataba bandari yatiwa saini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HATIMAYE Serikali ya Tanzania na Mamlaka ya Dubai kupitia kampuni ya DP World zimetia saini mikataba mitatu ya uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam, huku Rais Samia Suluhu Hassan akisema maslahi ya nchi yamezingatiwa na hakuna sauti iliyopuuzwa.

Makubaliano hayo ni ya mkataba wa nchi mwenyeji, mkataba wa upangishaji ardhi na mkataba wa uendeshaji bandari wa gati namba nne hadi saba.

Kabla ya kutiwa saini mikataba hiyo, Serikali ya Tanzania iliingia makubaliano na Mamlaka ya Dubai kuhusu uwekezaji huo (IGA) ambayo yalikosolewa na wadau mbalimbali, lakini ikasisitiza mkataba huo utakuwa na manufaa makubwa kwa nchi.

Mikataba hiyo imetiwa saini kutokana na kukamilika kwa mazungumzo ya pande hizo mbili baada ya kutiwa saini IGA kuhusu uwekezaji huo Oktoba 24 mwaka jana.

Akizungumza jana Ikulu Chamwino mkoani Dodoma wakati wa hafla ya utiaji saini mikataba hiyo iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, vyama vya siasa na dini, Rais Samia alisema sheria za Tanzania zitatumika katika utekelezaji wa mikataba hiyo.

Kwa mujibu wa Zuhura Yunus, Mkurugenzi wa Mawasiliano, Ofisi ya Rais, Ikulu, mikataba hiyo mitatu imetiwa saini kwa kuzingatia Kifungu cha 2 cha Sheria ya Ubia Na. 6 ya Mwaka 2023 na Kifungu cha 2 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 5 ya mwaka 2023.

Rais Samia alisema: "Ninataka niwahakikishie kuwa au niwape uhakika Watanzania wote kwamba maslahi mapana ya nchi yetu yamezingatiwa."

Alisisitiza kuwa serikali imesikiliza maoni ya vyama vya kisiasa, viongozi wa dini, viongozi wa serikali wastaafu, Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), asasi za kiraia, wanaharakati huru, vyombo vya habari na maoni katika mitandao ya kijamii.

"Bandari ya Dar es Salaam ni maliasili, ni jaha, ni hidaya, ni adhimu tuliyojaliwa na Mwenyezi Mungu. Bandari hii pia ni lango la biashara la nchi zinazotuzunguka. Bandari hii kuumbwa na kuwekwa kwetu Tanzania inatupa wajibu wa kuhudumia nchi jirani zinazoitegemea," alisema.

Rais alisema Watanzania wote wanakubaliana kuwa bandari kuna tatizo la uendeshaji na wapo wanaoamini Tanzania inaweza bila mbia.

"Ni mawazo mazuri ya kimapinduzi, lakini yapo mbali na uhalisia. Na njia hiyo itatuchukua muda mrefu sana kufika wakati Dunia inakwenda mbio. Sisi tungekuwa bado tunasota. Na isitoshe tulishajaribu, lakini hatukufanikiwa," alisema.

Mkuu wa Nchi alisema busara ziliwaelekeza kupata mwekezaji na si tu kujibu changamoto za upatikanaji mizigo au mzigo wa kutosha kuingia na kutoka nchini, bali kuongeza ufanisi utakaofanya gharama kuwa shindani na bandari zingine katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Bara la Afrika.

"Ukweli ni kuwa sisi sio mlango bahari pekee Mashariki na Kusini mwa Afrika, kuna milango bahari mitatu ambayo ni Mombasa, Beira na Durban, lakini upande wa Magharibi kuna milango ya bahari ya Walvis Bay na Lobito. Maana yake ni kwamba wanaotaka mizigo yao ifike, wana uwezo wa kuchagua bandari yoyote wakaitumia.

"Kinachotupa sisi turufu dhidi ya washindani wetu ni bahati ya mlango bahari wetu kuwa na masafa mafupi kuingia nchi za jirani na tunafikika na nchi nyingi kwa kutumia mpaka mmoja tu kulinganisha na milango bahari mingine. Ukaribu pekee si hoja ya kutosha, hivyo ni muhimu kuangalia ufanisi kwani wafanyabiashara hutazama pia ufanisi na gharama," alisema.

### DK. MPANGO

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisema takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) zinaonesha asilimia 26 ya Watanzania wanaishi chini ya kiwango cha umaskini.

"Kwa hesabu rahisi, Watanzania wasiopungua milioni 13 wanaishi katika umaskini, lakini wakati huohuo Mwenyezi Mungu aliipendelea nchi yetu kwa idadi kubwa ya watu na rasilimali nyingi za kila aina zikiwamo bandari.

"Umaskini wa watu wetu hauendani na upendeleo ambao Mungu ametupatia kwa wingi wa rasilimali. Katika mipango yetu tumeazimia taifa tulipeleke lenye kiwango cha juu cha kati cha kipato haraka iwezekanavyo ili tuweze kuwatoa wenzetu kwenye umaskini," alisema.

Dk. Mpango alisema ni vigumu kuwatoa katika umaskini wananchi bila rasilimali za nchi kuzifanyia kazi, akibainisha kuwa bandari imejaa ushindani mkali.

Aliagiza watendaji watakaopewa jukumu la kusimamia mikataba hiyo, waisimamie kwa uzalendo wa hali ya juu ili Tanzania inufaike.

### UFANISI BANDARINI

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa, alisema kuwa pamoja na kuchukua hatua mbalimbali za maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam, ufanisi katika utoaji huduma za bandari haujafikia viwango vinavyotakiwa kimataifa.



"Hali ya sasa ya utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam imeendelea kuwa ya kiwango cha chini kulinganishwa na bandari shindani kikanda. Kwa mfano, meli nyingi husubiri nangani kwa muda mrefu kabla ya kuhudumiwa.

"Leo hii, kuna meli 30 zilizofika bandarini zikisubiri kuingia bandarini kushusha mizigo wakati zile zinazohudumiwa gatini ni jumla ya meli 11. Wastani wa meli kusubiri nangani kwa Bandari ya Dar es salaam ni siku tano kulinganishwa na siku 1.25 kwa Bandari ya Mombasa na siku 1.6 kwa Bandari ya Durban," alisema.

Alibainisha kuwa ufanisi huo mdogo umetokana na changamoto mbalimbali zikiwemo kukosekana mifumo ya kisasa ya TEHAMA, kutokuwapo maeneo ya kutosha ndani na nje ya bandari kwa ajili ya kuhifadhi shehena ya mizigo na uchache wa magati au maegesho ya meli.

Pia kukosekana mitambo ya kutosha na ya kisasa ya kuhudumia shehena ambayo teknolojia yake inabadilika mara kwa mara na ina gharama kubwa ya uwekezaji na uendeshaji.

Mkurugenzi huyo alisema athari za kutokuwa na ufanisi katika Bandari ya Dar es Salaam ni pamoja na meli kusubiri muda mrefu nangani ambako kunasababisha kuongezeka kwa gharama ya kutumia Bandari ya Dar es Salaam.

Alitoa mfano kuwa gharama za meli kusubiri nangani kwa siku moja ni takriban Dola za Marekani 25,000 sawa na Sh. milioni 58 kwa siku.

"Meli kutumia muda mrefu kupakia na kupakua shehena gatini kwa wastani wa siku tano kulinganishwa na siku moja inayokubalika kimataifa; meli kubwa kutokuja katika Bandari ya Dar es Salaam kutokana na kuchukua muda mrefu kuhudumiwa," alisema.

Alibainisha kuwa hali hiyo husababisha bandari hiyo kuwa inayolishwa shehena na bandari nyingine na hivyo kuongeza gharama ya kutumia bandari hiyo na kuikosesha nchi mapato ambayo yangeweza kutumika katika utekelezaji miradi mikubwa ya kimkakati nchini ambayo ingesaidia kukuza uchumi na kuboresha huduma za wananchi.

"Pia, hali hii ya kukosekana kwa ufanisi inaongeza gharama katika mnyororo mzima wa usafirishaji kutoka nje ya nchi kupitia katika bandari yetu kwenda nchi za jirani zinazotumia bandari hiyo.

> **"Lile dude lililoleta maneno mengi limetoa sasa mikataba hii mitatu kama ilivyoridhiwa na Bunge na mikataba hii ilishasemwa."**

"Kwa mfano, gharama ya kusafirisha kasha moja kutoka nje ya nchi (on transit) kwenda nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zinafikia takriban Dola za Marekani 12,000," alifafanua.

Kwa kutambua hilo, mkurugenzi huyo alisema serikali pekee haitaweza kutatua changamoto zilizopo kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Kuanzia miaka ya 2000, serikali ilianza kushirikisha sekta binafsi na iliingia mkataba wa upangaji na uendeshaji na Kampuni ya Kimataifa ya Uendeshaji wa Vitengo vya Makasha, Hutchison ya Hong-Kong China kupitia Kampuni ya TICTS. Ni mkataba uliodumu kwa miaka 22 kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2022.

### KWANINI DP WORLD?

Alisema kampuni nyingi zilionesha nia ya kuendesha Bandari ya Dar es Salaam, lakini TPA iliingia makubaliano na Kampuni ya DP World kutokana na uzoefu wake katika uendeshaji wa shughuli za bandari barani Afrika, Asia, Ulaya na Amerika ya Kaskazini na Kusini.

"Kampuni hiyo pia, ina utaalamu wa kuchagiza mnyororo mzima wa usafirishaji kutoka maeneo ambayo bidhaa zinatoka mpaka kufika kwa walaji. Pia, uendeshaji wa maeneo maalum ya kiuchumi karibu na bandari, usafirishaji baharini na nchi kavu (kupitia njia ya reli), uwekezaji mkubwa katika maeneo mbalimbali ambayo imewekeza pamoja na kuajiri wazawa katika maeneo hayo,"alisema.

Alibainisha kuwa gati namba 0 hadi 3 katika Bandari ya Dar es Salaam yatatumiwa kwa pamoja baina ya Kampuni ya DP World na Serikali kupitia TPA kwa ajili ya shughuli zingine za kibiashara na serikali.

"Hapo awali, serikali ilikuwa inatumia takribani asilimia 90 ya mapato yaliyokusanywa katika uendeshaji wa maeneo hayo yaliyokodishwa na kubakiwa na asilimia 10 tu ya mapato yote. Hivyo, kutokana na mikataba hii, serikali itaweza kubaki na asilimia 60 ya mapato yote kutokana na gharama zote za uendeshaji kubakia kwa kampuni ya DP World," alisema.

Alifafanua kuwa wanatarajia mapato yanayokusanywa na TRA yataongezeka kutoka Sh. trilioni 7.8 za mwaka 2021/22 kwa mwaka hadi Sh. trilioni 26.7 kwa mwaka ifikapo mwaka 2032/33.

Alisema mkataba huo ukomo wa miaka 30 na utakuwa ukirejewa kila baada ya miaka tano ikiwa ni pamoja na kurejea mpango wa uwekezaji.

"Kutakuwa na kampuni ya uendeshaji ambayo TPA itamiliki hisa, kuwekwa kwa viwango vya utendaji mwekezaji anapaswa kuvifikia na watumishi wa sasa wa TPA wamepewa nafasi ya kuchagua kubaki TPA au kuhamia kwa mwekezaji.

"Jukumu la ulinzi na usalama katika eneo lote la bandari na yaliyokodishwa kwa kampuni DP World yataendelea kubaki serikalini na mwekezaji atalipa kodi na tozo zote za serikali kwa kuzingaia sheria za Tanzania," alisema.

### DOLA MIL. 250

Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya DP World, Sultan Ahmed Bin Sulayem, alisema wataanza kwa kuwekeza Dola za Marekani milioni 250 kuboresha bandari hiyo.

Alisema uwekezaji utafikia Dola za Marekani bilioni moja pamoja na uendelezaji wa maeneo mengine ya shughuli za bandari.

# Kilichombeba Makonda uteuzi CCM



**Na Beatrice Shayo**

HALMASHAURI Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) imefanya mabadiliko madogo ya sekretarieti kwa kumteua Paul Makonda kuwa Katibu wa Itikadi na Uenezi, akichukua nafasi ya Sophia Mjema.

Jana Rais Samia Suluhu Hassan alimteua Sophia kuwa mshauri wa Rais masuala ya wanawake na makundi maalum.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na kutiwa saini na Sophia, Halmashauri Kuu ya chama ilikutana jana jijini Dodoma katika kikao maalum chini ya Mwenyekiti, Rais Samia.

Taarifa hiyo pia ilibainisha kuwa Halmashauri Kuu imemteua Rabia Abdallah Hamid kuwa Katibu wa Halmashauri ya CCM Taifa, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI), akichukua nafasi ya Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Uhusiano wa Afrika.

"Pamoja na masuala mengine imeridhia kwa kauli moja kuelekeza serikali kuendelea na hatua ya utiaji saini mikataba ya uendelezaji na uwekezaji wa bandari," ilibainishwa katika taarifa hiyo.

**KILICHOMBEBA MAKONDA**

Naibu Katibu Mkuu Chama cha Wananchi (CUF) Tanzania Bara, Magdalena Sakaya, akizungumzia uteuzi wa Makonda, alisema miongoni mwa sababu zinazombeba ni utulivu katika uongozi.

Alisema viongozi wanaoteuliwa kushika nyadhifa tofauti na baada ya muda mfupi kuondolewa kunatokana na kukosa utulivu na kutoyasoma mazingira ya ofisi wanazokabidhiwa.

"Ukienda kwa hatua na kidogokidogo utakwenda kwa ufanisi na unapoingia katika taasisi yoyote ngeni ni lazima uisome kwanza, haitakiwi kukurupuka na kujiona mjuaji sana. Utaweza kutamka kitu hata sicho," alisema Sakaya.

Alisema Makonda anastahili kuchukua nafasi ya Sophia kwa kuwa alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alitumia nafasi yake kuisaidia jamii na akionekana msaada hasa kwa makundi ya kinamama.

"Makonda alikuwa na misimamo yake na binadamu hawezi kuwa sawa kila mahali, hivyo awamu yake akiwa Mkuu wa Mkoa alifuatilia kinamama waliotelekezwa watoto, alihakikisha kinamama ambao wanapata mikopo, wajasiriamali wapate maeneo ya kufanyia biashara" alisema Sakaya

Mchambuzi wa masuala ya siasa, Luaga Kizoka alimpongeza Rais Samia kwa kumpa nafasi hiyo Makonda, akiamini ataleta ushawishi mkubwa kwa vijana kukipigia kura chama hicho katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwakani.

Alisema asilimia kubwa ya wapigakura ni vijana, akitolea mfano wa takwimu za mwaka 2020 zinaonesha asilimia 70 ya wapigakura walikuwa vijana, hivyo kumweka kijana katika nafasi hiyo kutaongeza chachu ya ushiriki wa vijana katika uchaguzi ujao.

"Makonda ni kijana, kwahiyo anaweza kusikia sauti za vijana wenzake akawaelewa. Ni lazima tupate viongozi ambao ni wasikivu na mimi nina imani kabisa kuwa Makonda ni msikivu kwa sauti za vijana," alisema.

Mchambuzi mwingine wa siasa, Hamduni Maliseli alisema Rais Samia hajakosea kumteua Makonda katika nafasi hiyo kwa kuwa ni mtu mwenye uwezo na ushawishi mkubwa katika chama.

Alisema kupitia uteuzi huo (Makonda) atakwenda kukiunganisha chama na kuondoa dhana aliyoiita ya makundi iliyojitokeza.

Alisema kiongozi huyo ni mmoja kati ya watendaji wazuri katika chama hicho. Aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Chipukizi na kuifanya kazi hiyo vizuri, alijishughulisha na "siasa za chinichini"

"Makonda anaifahamu mifumo ya chama, siyo tu katika kuiunda bali hata kuitekeleza misingi yake ya awali. Ni miongozi mwa vijana ambao wapo tayari kufa kwa chama. Ni miongoni mwa wanachama kindakindaki wa CCM" alisema.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mrema alisema: "Ni uteuzi wa kushangaza kwamba CCM imeona miongoni mwa wanachama wake wote mwenye uwezo wa kukisemea chama chao ni Makonda, ambaye rekodi yake inafahamika alipokuwa Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam, iliyopelekea akatumbuliwa."

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, kupitia ukurasa wake wa X, alimkaribisha Makonda mara tu baada ya kuteuliwa na kumtakia kila la kheri kwenye majukumu yake hayo ambayo waziri huyo aliwahi kuyatumikia.

"Mdogo wangu Paul, Karibu sana kwenye uongozi wa juu kabisa wa chama chetu. Nina hakika umetumia vizuri muda wa likizo, and now you are ready for the job (na sasa uko tayari kwa kazi)! HONGERA kwa kuaminiwa na nakutakia kila la kheri!" aliandika Waziri Nape.

***Imeandaliwa na Beatrice Shayo, Christina Mwakangale, Elizabeth Zaya na Jeniffer Gilla**


TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

**TAARIFA KWA UMMA**

**TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI**

**Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)** inapenda kuwataarifu waombaji kazi waliofaulu mtihani wa mchujo na kuchaguliwa **(SELECTED)** kwa ajili ya usaili wa vitendo na mahojiano **(Practical and Oral Interview)** unatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe **29 Oktoba, 2023** hadi tarehe **2 Novemba, 2023** na hatimaye kuwaajiri watakaofaulu usaili huo. Wasailiwa wanaoitwa kwenye usaili wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo: -

i. Kila Msailiwa anapaswa kuwa na **kitambulisho** kwa ajili ya utambuzi; vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na:- Kitambulisho cha Taifa, Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, Kitambulisho cha Mpiga kura, Hati ya kusafiria au Leseni ya udereva;
ii. Wasailiwa wanatakiwa kufika na **vyeti vyao halisi, kuanzia cheti cha Kuzaliwa, Kidato cha IV, VI, Astashahada, Stashahada, Stashahada ya Juu, Shahada** na kuendelea kutegemeana na sifa za mwombaji;
iii. Wasailiwa watakaowasilisha **"Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati za matokeo za Kidato cha IV na VI (Form IV and Form VI result slips) HAZITAKUBALIWA NA HAWATARUHUSIWA KUENDELEA NA USAILI;**
iv. Kila msailiwa atajigharamia kwa chakula, usafiri na malazi;
v. Kila msailiwa azingatie **tarehe** na **mahali** alipopangiwa kufanyia usaili kulingana na ratiba husika na muda wa kufika ni **saa moja kamili asubuhi**;
vi. Kwa waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe Vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika **(kama TCU, NACTE au NECTA)**;
vii. Waombaji kazi ambao namba zao hazikuchaguliwa kwa ajili ya hatua inayofuata watambue kuwa hawakukidhi vigezo. Hivyo, wasisite kuomba tena pindi nafasi za kazi zitakapotangazwa na kuzingatia mahitaji ya tangazo husika.
viii. **Kwa kada ambazo wanatakiwa kusajiliwa na Bodi zao za Kitaaluma wanapaswa kuja na vyeti vyao Halisi vya Usajili pamoja na Leseni za kufanyia kazi (zilizo hai).**
ix. **Wasailiwa wote walioitwa kwenye usaili wahakikishe wanaingia kwenye akaunti zao na kunakili namba ya mtihani kwa kuwa namba hizo hazitatolewa siku ya usaili.**
x. Matokeo na ratiba ya usaili vinapatikana kupitia tovuti ya TRA www.tra.go.tz

Kwa taarifa zaidi, tembelea ofisi za TRA zilizopo karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| Tovuti | : | **www.tra.go.tz** |
| Namba za simu bila malipo | : | **0800-780 078** au **0800-750 075 au 0800-110 016** |
| WhatsApp | : | **0744 23 33 33** |
| Barua pepe | : | **huduma@tra.go.tz** au **services@tra.go.tz** |

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;
**Idara ya Usimamizi wa Rasilimali Watu na Utawala**



Mbunge wa Newala Vijijini, Maimuna Salum Mtanda (wa pili kulia) akimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation na Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Esther Mwambapa (wa pili kushoto) alipopokea pikipiki 5 zenye thamani ya shilingi milioni 15 pamoja na mfano wa hundi yenye thamani ya shilingi milioni 20 ambazo ni mtaji wezeshi kwa wanachama wa vikundi vya BUTA Vicoba kwenye Mkutano Mkuu wa nne wa Mwaka wa BUTA Vicoba uliofanyika mwishoni mwa wiki katika Viwanja vya Sabasaba mjini Newala mkoani Mtwara. Kushoto ni Mkurugenzi wa Taasisi ya BUTA Vicoba, Semeni Gama. **PICHA:MPIGAPICHA WETU.**

MTIHANI DARASA LA IV

# Polisi kumwekea ulinzi mwanafunzi anayedaiwa kunajisiwa na baba yake

**Na Halfani Chusi**

MTOTO aliyedaiwa kunajisiwa na baba yake kwa miaka mitatu mfululizo, anatarajiwa kurejeshwa mkoani Dodoma leo ili afanye Mtihani wa Taifa wa Darasa la IV uliopangwa kufanyika juma hili.

Akiwa Dodoma, mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka tisa, atakuwa chini ya uangalizi wa Jeshi la Polisi mkoani humo kutokana na utata uliotawala tukio la kutoroka kwa baba yake akiwa mahabusu ya Kituo cha Polisi Mvumi, wilayani Chamwino.

Baba wa mtoto huyo, Daniel Simle, mkazi wa Kijiji cha Ilewelo, Kata ya Manzase wilayani Chamwino, alikamatwa na polisi Julai 30 mwaka huu kwa tuhuma za kumnajisi mwanawe huyo kwa miaka mitatu mfululizo, lakini akadaiwa kutoroka siku mbili baadaye akiwa katika mahabusu ya kituo tajwa cha polisi.

Kutokana na tukio hilo, Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma lilimkabidhi mtoto huyo kwa mama yake mzazi, Sukaina (jina la pili tunalo) anayeishi Tabata, jijini Dar es Salaam. Sukaina aliondoka Dodoma Agosti 3 mwaka huu akiwa na mwanawe huyo ambaye ni mwanafunzi wa darasa la IV katika Shule ya Msingi Ilewelo, wilayani Chamwino.

Sukaina amemwambia mwandishi wa habari hizi kuwa Mtihani wa Taifa wa Darasa la IV mwaka huu umepangwa kufanyika kwa siku mbili (Jumatano na Alhamisi wiki hii), hivyo amelazimika kumrejesha mwanawe Chamwino alikoandikishwa kufanya mtihani huo.

Sukaina anasema mtuhumiwa kutoroka akiwa mikononi mwa polisi kunampa hofu ya usalama wake binafsi na mwanawe; huenda mtuhumiwa ataamua kufanya jambo baya dhidi yao ili kupoteza ushahidi.

"Ninaishi kwa hofu, mtuhumiwa hajulikani aliko. Mtoto anatakiwa kurudi Dodoma kufanya Mtihani wa Taifa wa Darasa la IV. Kama sitokuwa na ulinzi, mtoto hatafanya mtihani huu kwa sababu kule mimi nimeshakuwa adui.

"Ingekuwa mtuhumiwa amepatikana, ningekuwa na amani. Hata sasa huku Dar es Salaam, kuna shule anasoma kwa muda, ninalazimika kumsindikiza mwanangu shuleni na kumsubiri kila siku. Ni kama na mimi sasa ni mwanafunzi, tunasoma wote! Hata muda wa kutafuta fedha kwa ajili ya matumizi ninakosa.

"Ninaogopa kumwacha aende peke yake kwa sababu hapa Dar es Salaam ninapokaa, mtuhumiwa anapajua. Hofu yangu anaweza kumvizia mwanangu akamfanyia kitu kibaya au kumuua kabisa ili apoteze ushahidi katika kesi yake.

"Ninaiomba serikali na Jeshi la Polisi kumtafuta huyo mtuhumiwa ili akajibu mashtaka (tuhuma) yanayomkabili ya kubaka (kunajisi) mtoto wake wa kumzaa," Sukaina anasema.

Mama huyo pia analiomba Jeshi la Polisi mkoani Dodoma kumpa ulinzi yeye na mwanawe watakapokuwa Chamwino kwa ajili ya mtoto wake kufanya mtihani huo.

"Kama nitampeleka huko bila kuwa na ulinzi, usalama wetu utakuwa mdogo sana. Tunaweza hata kudhuriwa na mtuhumiwa au watu wengine anaoshirikiana nao," anadai.

**KUTOKA POLISI**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi Martin Otieno, alipotafutwa na mwandishi kuzungumzia suala hilo mwishoni mwa wiki, alisema mtuhumiwa huyo hajakamatwa. Wanaendelea kumsaka.

"Hatujamkamata, lakini anafuatiliwa, atakamatwa tu! atarukaruka tu, lakini ipo siku atanasa tu," Kamanda Otieno alisema.

Kuhusu usalama wa mtoto na mama yake watakapokuwa mkoani Dodoma juma hili, Kamanda Otieno alisema:

"Huyo mama amlete tu huyo mtoto wake kufanya mtihani, asiwe na shaka yoyote, tutampa ulinzi. Kutakuwa na askari wa kike atamsindikiza na atamsubiri mpaka atakapomaliza mtihani kisha atampeleka mpaka katika kituo cha mabasi kurejea Dar es Salaam baada ya mtihani.

"Kwahiyo, asiwe na wasiwasi, amlete tu mtoto kufanya mtihani. Tutahakikisha wanakuwa salama tangu wanapofika huku na kwenye mizunguko yao yote."

**UONGOZI SHULENI**

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ilewelo, Selina Mkwela, anasema ana taarifa za ukatili dhidi ya mwanafunzi wake huyo anayemtaja alikuwa na uwezo mkubwa darasani.

Katika mitihani shuleni, Mwalimu Mkuu Selina anasema jina la mtoto huyo halikukosekana kwenye orodha ya wanafunzi 10 bora. Mwaka huu shule hiyo ina watahiniwa 48 wa Mtihani wa Taifa wa Darasa la IV.

Mwalimu Mkuu Selina anasema ameshawasiliana na mama wa mtoto huyo na kuandaa mazingira mazuri kumwezesha kufanya mtihani huo.

Kimsingi, ukatili dhidi ya mtoto huyo ni kwenda kinyume cha Lengo Na. 5 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalozitaka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhakikisha zinafikia usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana.

Kwa siku mbili mfululizo, mnamo Septemba 2 na 3 mwaka huu, Nipashe ilichapisha ripoti maalum kuhusu mkasa wa mtoto huyo kudaiwa kunajisiwa na baba yake mzazi kwa miaka mitatu mfululizo huku polisi wakidai mtuhumiwa huyo kutoroka akiwa katika mahabusu yao wilayani Chamwino.

# Wadau walivyoupokea mkataba wa Bandari

**Na Waandishi Wetu**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi na Maendeleo ya Ujasiriamali (IMED), Dk. Donath Olomi, ameipongeza serikali kwa hatua iliyofikia ya kushirikiana na sekta binafsi katika kuboresha huduma bandarini.

Alisema baada ya kuingiwa kwa mkataba huo ushirikiano wa viwango vya utoaji huduma vitaboreka, ikiwamo kasi ya utoaji mizigo itakayochochea ongezeko la mizigo itakayoingia nchini kupitia bandari hiyo na kuipatia nchi mapato zaidi.

"Kwa sababu tukizembea katika kuboresha huduma za bandari, kitakachotokea utashangaa mizigo inatoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) inaenda Angola na kuiacha bandari yetu ikiwa haina biashara," alisema Olomi.

Alisema pia anategemea kupitia ushirikiano huo mifumo ya kutoa huduma itaunganishwa vizuri na isomane kati ya taasisi zinazohusika na utoaji mizigo katika bandari hiyo, jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa na watumiaji wa bandari kama mojawapo ya changamoto ya miaka mingi.

Alisema pia anategemea ushirikiano huo utapunguza changamoto ya gharama kubwa za kusafirisha mizigo kutoka nchi mbalimbali kupitia Bandari ya Dar es Salaam, hali inayosababisha viwanda kutumia gharama kubwa katika uzalishaji na matokeo yake bidhaa kuuzwa bei ya juu.

Mchambuzi wa uchumi, Profesa Haji Semboja, alisema utiaji saini ni shughuli za seriklai kwa niaba ya wananchi.

"Baada ya kutia saini kinachofuata ni utekelezaji wa mkataba unakuwaje? Nafikiri hoja kubwa ya wananchi ni kwamba maendeleo haya siyo ya watu wengine isipokuwa yawe ni ya wananchi wote," alisema na kuongeza:

"Utaribu nzima wa mpango wa utekelezaji wa mkataba wenyewe wahusika kila wakati wanatakiwa kuelewa vitu gani wananchi walikuwa wanavizungumzia na vile ambavyo walikuwa na wasiwasi navyo, naamini ni wasikivu watafuata vizuri na wananchi wakishajua suala la bandari litakuwa na maendeleo na wenyewe watajitahidi katika maeneo yao kuongeza nguvu na jitihada waweze kuzalisha na bandari itumike kwa maendeleo."

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shule Kuu Elimu (DUCE), Dk. George Kahangwa, alisema anaamini kwamba hatua ya serikali kufikia uamuzi huo ni kwamba maoni ya wananchi yamezingatiwa.

"Ila sote tu mashahidi mkataba umesainiwa katika muktadha wa kwamba wapo Watanzania waliotoa maoni ya usainiwe na wapo waliopinga. Yamkini sauti za walioulalamikia zimesaidia kiasi. Dondoo zinasema utaweza kuvunjwa na hauhusishi bandari zote," alisema Dk. Kahangwa.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabishara Tanzania (JWT), Khamis Livembe, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusaini mkataba wenye lengo la kunufaisha taifa na wafanyabishara kwa ujumla.

Alisema suala la bandari lilikua ni kilio cha muda mrefu cha wafanyabishara wengi nchini, hali iliyosababisha kuwapo kwa mabadiliko ya mara kwa mara ya watendaji wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Alisema hali hiyo bado haikuridhisha kwasababu bado waliendelea kupata shida na hata kuwafanya wafanyabishara kushusha mizigo mwenye bandari za nchi jirani ikiwamo Kenya ili kupunguza ucheleweshaji wa kupakua mizigo, ufanisi mdogo na mizigo kupotea.

"Kwa uwekezaji huu kutasaidia sana kuinua biashara zetu, kupunguza biashara za kushusha mizigo na gharama za usafiri kutokana na urahisi wa kushusha mizigo hiyo," alisema Livembe.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wakala wa Forodha Zanzibar na mjumbe wa JWT, Omary Hussein, alisema mkataba ambao Rais Samia ameusaini ni wa kufungua milango ya kibiashara na kiuchumi.

Alisema kwa upande wa Zanzibar watanufaika na kusainiwa kwa mkataba huo kwasababu walikuwa wakitumia zaidi Bandari ya Mombasa kushusha mizigo yao na kwa maboresho hayo watatumia Bandari ya Dar es Salaam.

Omary alisema: "Tumpongeze Rais Samia kwa maono yake makubwa yanayofungua uchumi wa Taifa na kurahisisha shughuli za kibiashara nchini kupitia TPA na kurahisisha shughuli za uwekezaji nchini, tunamshukuru na kumpongeza sana".

Mwanasiasa mbobezi, James Mbatia alisema: "Suala hili la mkataba lilikuwa janga kubwa na niipongeze serikali imejitahidi kwa kiasi kikubwa kuweka nguvu kwenye kinga kuliko tiba... imesikiliza na kuchukua maoni mengi ya wananchi."

"Niwapongeze wale wote waliojitokeza mstari wa mbele kupaza sauti zao na kupambana katika jambo hili..ila niiombe serikali yale yote ambayo imeyasema ikiwamo masuala ya local content ijitahidi kuyatekeleza na kuyasimamia na yaingie kwenye mkataba mkubwa ili baadaye tusije kujiingiza kwenye shida."

***Imeandaliwa na Jenifer Gilla, Beatrice Shayo, Mary Geofrey na Elizabeth Zaya**

TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA [MAHESABU YALIYO KAGULIWA]

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## TANZANIA COMMERCIAL BANK PLC

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Mwaka wa Sasa 31-Dec-22 | Mwaka Uliopita 31-Dec-21 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 53,562 | 49,972 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 60,390 | 16,522 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 103,442 | 133,175 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 69,127 | 73,882 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 271 | 284 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 96,804 | 124,636 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 841,590 | 718,600 |
| 12 | Mali Nyingine | 43,162 | 41,047 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 20,610 | 22,599 |
| | Haki ya matumizi ya mali | | |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,288,958** | **1,180,715** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 862,393 | 738,724 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 124,778 | 178,978 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 2,207 | 3,967 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 20,780 | 1,502 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 2,641 | 8,362 |
| 27 | Dhima Nyingine | 30,127 | 27,057 |
| 28 | Madeni | 129,401 | 108,912 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,172,328** | **1,067,502** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **116,631** | **113,213** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,372 | 28,072 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 72,411 | 65,567 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 3,154 | 9,141 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 9,694 | 10,433 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **116,631** | **113,213** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 151,019 | 207,028 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 72,800 | 80,859 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 15,323 | 15,554 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 235 | 11 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.05% | 9.59% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.43% | 10.94% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 87.44% | 80.52% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 65.29% | 69.20% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 80.83% | 82.70% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 7.57% | 14.27% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 9.17% | 13.13% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Limbikizo la Mwaka Mwaka Wa Sasa 31-Dec-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-21 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 139,782 | 135,178 |
| 2 | Gharama za Riba | (48,570) | (39,787) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **91,213** | **95,391** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | **(1,758)** | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (13,945) | (13,669) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **32,818** | **34,506** |
| | 6.1 Faida/(Hasara) zitokanazo na miamala ya Fedha za Kigeni | 4,138 | 2,246 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 19,352 | 26,021 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 9,328 | 6,238 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(101,457)** | **(96,563)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 49,806 | 50,912 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 9,174 | 581 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 42,478 | 45,070 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **6,871** | **19,665** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 3,717 | 10,498 |
| 10 | **Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **3,154** | **9,167** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | **630** | **(253)** |
| | 11.1 Hasara ya sasa kutoka kwa wajibu wa faida | 901 | (362) |
| | 11.2 Kodi kadirio la mbeleni la mafao ya mtumishi | (270) | 108 |
| | 11.3 Gharama ya zamani juu ya wajibu wa faida | - | - |
| | 11.4 Kodi iliyopungua kwa gharama ya zamani kwenye wajibu unaofafanuliwa | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **3,784** | **8,914** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 1,086 | 1,091 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 101 | 326 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | 48 | 47 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.25% | 0.75% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.70% | 7.87% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 58.78% | 74.34% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 8.95% | 9.77% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-21 |
|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 6,871 | 19,665 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | - Hasara Katika Mali | 25,966 | 13,913 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (136,740) | (102,603) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | 4 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 82,874 | 114,617 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (50,046) | (22,531) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 3,195 | (12,704) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (235) | 2,505 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (9,459) | (7,800) |
| | - Kodi kadirio la mbeleni la mafao ya mtumishi | (618) | (529) |
| | - Gharama ya mafao ya mtumishi | 1,766 | 1,137 |
| | - Mengineyo (Mapato ya ruzuku & hifadhi nyingine) kutoka muunganiko wa biashara ) | (229) | 85 |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | ***(76,655)*** | ***5,759*** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (2,330) | (7,709) |
| | Ununuzi wa Mali Zisizoonekana | (577) | (855) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | ***(2,907)*** | ***(8,563)*** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Fedha Taslimu iliyolipwa kwenye kodi ya share za bonasi | (367) | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Malipo ya Dhima ya Kukodisha | (6,151) | (6,791) |
| | Mengineyo (Kodi katika Hisa za Ziada &Ruzuku Iliyopokelewa) | 93 | 267 |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | ***(6,425)*** | ***(6,524)*** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(85,987)** | **(9,329)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 111,197 | 120,526 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **25,211** | **111,197** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Mafao yanayoelezeka | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | **-** | **77,600** | **(2,891)** | **739** | **-** | **9,694** | **113,213** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | - | | - | - | - | - |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 3,154 | | - | - | - | **3,154** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | 630 | | - | - | - | **630** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | | - | - | - | - |
| Hisa za ziada | - | - | - | | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 739 | | (739) | - | - | - |
| Fedha Taslimu iliyolipwa kwenye kodi ya share za | - | - | (367) | | - | - | - | **(367)** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yalifafanuliwa baada ya | - | - | - | | - | - | - | - |
| Kurudishwa kwa Gawio lililosimamishwa mwaka 2017 | 3,300 | - | (3,300) | | - | - | - | **0** |
| Mengineyo | - | - | - | | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,372** | **-** | **78,456** | **(2,891)** | **-** | **-** | **9,694** | **116,631** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | **-** | **69,172** | **(2,638)** | **-** | **-** | **9,694** | **104,299** |
| **Mabadiliko ya IFRS 9** | - | - | - | | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya udhibiti | - | - | - | | - | - | - | - |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 9,167 | (253) | - | - | - | **8,914** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | | - | - | - | - |
| Hisa za ziada | - | - | - | | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (739) | | 739 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | | - | - | - | - |
| **Gawio lililolipwa** | - | - | - | | - | - | - | - |
| faida ya sasa ya manufaa yalifafanuliwa | - | - | - | | - | - | - | - |
| Hamisho kutoka/kwenda hifadhi ya udhibiti | - | - | - | | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | **28,072** | **-** | **77,600** | **(2,891)** | **739** | **-** | **9,694** | **113,213** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA, 2022

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| **MR.S.K.MOSHINGI**<br>Ofisa Mtendaji Mkuu | Imesainiwa | **09.10.2023** |
| **MS. REGINA E. SEMAKAFU**<br>Mkurugenzi wa Fedha | Imesainiwa | **09.10.2023** |
| **MR. S. NYENYEMBE**<br>Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani | Imesainiwa | **09.10.2023** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA**<br>Mwenyekiti wa Bodi | Imesainiwa | **09.10.2023** |
| **MR. GILBERT W. CHAWE**<br>Mjumbe wa Bodi | Imesainiwa | **09.10.2023** |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba haijaisha mpaka iishe, nusu fainali AFL inawezekana

**KESHO** wawakilishi pekee wa Ukanda wa Afrika Mashariki (CECAFA), Simba, kwenye michuano ya African Football League watashuka dimbani ugenini nchini Misri kwenye mechi ya marudiano dhidi ya wenyeji wao, Al Ahly.

Timu hizo zinarudiana baada ya mchezo wa kwanza uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Ijumaa iliyopita kumalizika kwa sare ya mabao 2-2, hivyo mshindi wa mechi hiyo atatinga nusu fainali.

Michuano hiyo mikubwa kabisa na yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika inafanyika kwa mara ya kwanza ikijumuisha klabu kubwa nane na imeanzia hatua ya robo fainali.

Mbali na Simba na Al Ahly, klabu nyingine zinazoshiri michuano hiyo ni Wydad Casablanca (Morocco), Mamelodi Sundowns (Afrika Kusini), Esperance de Tunis (Tunisia), Petro Atletico de Luanda (Angola), Enyimba FC (Nigeria) na TP Mazembe ya DR Congo.

Kwa ujumla ni michuano migumu kutokana na kushirikisha timu nane bora zaidi Afrika, jambo ambalo Simba inapswa kujipanga vilivyo ili kuweza kupata matokeo mazuri ugenini na kusonga mbele.

Katika mechi hiyo ya marudiano, Simba inahitaji ushindi wowote ama sare kuanzia ya mabao 3-3 ili kutinga nusu fainali, jambo ambalo kimahesabu ni gumu hasa kutokana na ubora wa wapinzania wao, Al Ahly wakiwa nyumbani.

Lakini katika soka sisi tunaamini hakuna linaloshindikana na kinachotakiwa ni maandalizi makubwa hasa kwa kuwajenga wachezaji kisaikolojia kwa kuwakumbusha matukio makubwa ya mechi ambazo Simba iliwahi kufanya maajabu tena ikiwa ugenini.

Mojawapo ni mwaka 1979 katika raundi ya kwanza kwenye michuano ya Klabu Bingwa Afrika dhidi ya Mufulira Wanderers ya Zambia baada ya kufungwa mabao 4-0 hapa nchini, ilienda ugenini na kupindua meza kwa kuwachapa Wazambia hao 5-0 na kusonga mbele.

Na kama mfano huo ni wa muda mrefu basi mwingine unaoweza kuwaongezea morali ya upambanaji wachezaji wa Simba ni wa mwaka 2003, ambao Simba ikiwa ugenini nchini Misri iliwatupa nje mahasimu wa Al Ahly, Zamalek kwa mikwaju ya penalti 3-2 katika ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba ilitoa Zamalek baada ya kuifunga bao 1-0 hapa nchini na mechi ya marudiano nchini Misri wenyeji nao wakapata ushindi kama huo, hivyo kuingia katika changamoto ya mikwaju ya penalti na Wekundu wa Msimbazi kushinda 3-2.

Ikumbukwe pia kama mechi ya marudiano ya Simba dhidi ya Al Ahly ugenini, itamalizika kwa sare ya mabao 2-2, changamoto ya mikwaju ya penalti itachukua nafasi yake, jambo ambalo katika maandalizi ya Simba wanapaswa kulifanyia kazi.

Katika hilo, sisi tunaamini mechi hiyo haijaisha mpaka dakika 90 za pili zitakapomalizika zote pale jijini Cairo na Simba haipaswi kukata tamaa wala kwenda kinyonge katika mchezo huo wa marudiano kwa kuwa lolote linaweza kutokea katika soka kama wakiwa na ari ya upambanaji.

Kama iliweza kuitoa Mufulira na Zamaleki ugenini, kwa nini ishindwe kurudia rekodi hiyo wakati huu kikosi chake kikiundwa na wachezaji wengi wazoefu wa michuano ya kimataifa na ambao wameshacheza dhidi ya Al Ahly zaidi ya mara tatu? Kikubwa ni maandalizi makubwa ndani na nje ya uwanja na kujiamini wanaweza.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com







Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba ikivunja benki kwa kiungo mkabaji halisi itafika mbali CAF

**NADHANI** sasa ule mjadala wa kiwango cha Simba msimu huu ni kizuri au kibovu umemalizwa rasmi Ijumaa iliyopita ilipocheza mechi ya ufunguzi wa michuano ya African Football League dhidi ya Mabingwa wa Afrika, Al Ahly ya Misri.

Katika mechi hiyo iliyoisha kwa sare ya mabao 2-2, wageni mbalimbali mashuhuri waliosafiri maili nyingi kushuhudia mechi hiyo, walionyeshwa kufurahishwa.

Ilikuwa ni mechi kali, bora iliyokuwa na maana halisi ya mchezo mkubwa wa ufunguzi wa michuano hiyo. Awali kulikuwa na wasiwasi kwa baadhi ya mashabiki wa soka nchini hasa kuhusu kile kilichokuwa kikielezwa kiwango kisichoridhisha cha Simba msimu huu.

Baada ya mechi hiyo, mashabiki wengi wameonesha kuridhishwa na kiwango, pamoja na jinsi wachezaji walivyopambana, hata mfumo wa kocha Roberto Oliveira. Hakukuwa na mnyonge, timu zote kuna wakati zilionekana kutawala na kuna wakati zililazimika kurudi nyuma kuzuia mashambulizi ya timu pinzani.

Timu zote zilikosa mabao kwa nyakati tofauti, ila Al Ahly ndiyo iliyokosa mabao mengi ya wazi na nina uhakika kama yale yangekoswa na wachezaji wa Simba kelele zingekuwa nyingi.

Baada ya kuangalia mechi ile, kusikiliza mashabiki wa Simba wenyewe, Yanga na wadau mbalimbali, wote wanakubaliana kuwa kumbe kikosi ni kizuri, ila kingekuwa vizuri zaidi kama kingepata kiungo mkabaji halisi kutokana na mfumo wanaocheza.

Hili nilishawahi kulielezea siku za nyuma na nitaendelea kulisisitiza kuwa kikosi hiki cha Simba kinahitaji kiungo mkabaji halisi kama ilivyokuwa kipindi cha nyuma wakiwa na James Kotei, Gerson Fraga na Thadeo Lwanga.

Aina hii ya kiungo mwenye akili ya kukaba zaidi kuliko kushambulia ili kuwalinda mabeki wa kati na wa pembeni ndiyo tatizo linaloikabili Simba kiasi kwamba wanaruhusu mabao karibuni kila mechi inayocheza, iwe ya kimataifa kama ya Ijumaa, Ligi ya Mabingwa, Ligi Kuu Tanzania Bara, na hata za kirafiki.

Kinachoipa ushindi zaidi Simba ni kwa sababu ina viungo washambuliaji bora wenye uwezo wa kufunga pia na mastraika wazuri ambao wakishambulia mfululizo kuna uwezakano mkubwa wa kupata bao au mabao.

Lakini Simba hiyo hiyo inaposhambuliwa ni rahisi zaidi kufungwa bao kwa sababu wachezaji wake wote wa kukaba na kushambulia wana akili ya aina moja, kushambulia na kupiga pasi za mwisho zaidi kuliko kukaba.

Wanapopoteza mpira ndipo tabu inapoanza. Tumeona kwenye mechi dhidi ya Al Ahly ambapo ubora na udhaifu wa timu hiyo umeonekana.

Fabrice Ngoma na Sadio Kanoute ambao wote walicheza vizuri mno kwenye mechi hiyo, kiasili hata wanavyocheza tu, utagundua kuwa ni namba nane, yaani wanakwenda mbele kushambulia, halafu wanarejea nyuma kusaidia.

Hata Mzamiru Yassin asili yake ni namba nane, nafasi ya kiungo mkabaji alirejeshwa miaka ya hivi karibuni. Hawa wanatakiwa watafutiwe mtu mwenye uwezo wa 'kukitifua' pale kati, ambaye kazi yake itakuwa ni kutibua pasi za juu, mpenyezo, na kumzuia au kukabiliana na mchezaji yeyote ambaye atakuwa anafanya shambulizi la kujibu.

Inaposhambuliwa hasa kwa shambulizi la kurudishia 'counter attack', hapo ndipo utakapoona dhahiri pengo na udhaifu halisi wa Simba. Hata Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amekiri kuwa Simba inaruhusu mabao kwa makosa yao wenyewe na si ubora wa wapinzani.

Kama ina Henock Inonga na Che Malone Fondoh, wakitafutiwa mtu wa aina hiyo, nadhani inaweza kufika mbali kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa sababu kabla ya hatua ya makundi kuna kipindi cha usajili wa dirisha dogo, Simba inaweza kutumia kipindi hiki kusaka namba sita halisi popote pale ikiwezekana kuvunja hata mkataba wa klabu yake ili aongeze nguvu na kukifanya kikosi kiwe imara zaidi tofauti na sasa ambapo pamoja na kwamba kiko vizuri, lakini kinataabika kwa kukosa mtu wa 'kazi chafu' uwanjani.

# Wanafunzi zaidi ya 200 washinda shindano la Hisabati

**Na Gwamaka Alipipi**

CHAMA cha Hisabati Tanzania (CHAHITA), kimetoa orodha ya wanafunzi 233 kati ya 812 waliofanya vizuri katika shindano la Hisabati kitaifa lililoratibiwa na chama hicho.

Wanafunzi hao ni kutoka mikoa 11 ya Tanzania Bara na Zanzibar ambao walipata zaidi ya asilimia 40 ya alama zilizohitajika kwenye shindano hilo, wengine 579 wakipata chini ya kiwango hicho.

Akisoma matokeo hayo jana Dar es Salaam, Mwenyekiti wa CHAHITA, Betinasia Manyama, alitaja baadhi ya wanafunzi wa kundi la wanafunzi 10 bora wa jumla kidato cha tatu na nne akiwamo Stella Maliti wa Shule ya Marian Girls ya Pwani, Brown Mafuru wa Marian Boys Pwani na Alice Gonza wa Canossa ya Dar es Salaam.

Alisema mtihani huo ulihusisha makundi mawili, la kwanza likiwa ni wanafunzi wa kidato cha tatu hadi cha nne na la pili ni kidato cha tano hadi sita.

Betinasia alisema kupatikana kwa washindi hao kunatoa mwanya wa kupatikana kwa washiriki wanane katika shindano la hisabati ngazi ya Afrika Mashariki, Afrika na dunia litakalofanyika mwakani.

Kuhusu idadi ya shule zilizoshiriki alisema ni 58, wanafunzi wakiwa 540 na waliopata asilimia 40 na kuendelea walikuwa ni 167 na chini wastani huo ni 373.

Alisema kwa kidato cha tano na sita walioshiriki ni 272 kutoka shule za sekondari 22, wavulana wakiwa 162 na wasichana 110, takwimu zikionyesha walipata asilimia 40 na zaidi ni wanafunzi 66, wenye upungufu na wastani huo ni wanafunzi 206.

Betinasia alisema wanafunzi walioshika nafasi 10 za mwanzo ni Amosi Paulo wa Shule ya Sekonadri Mzumbe mkoani Morogoro, Elia Wambura wa Iyunga Technical Mbeya na Mwanaarab Said wa Shule ya Sekondari Lumumba Mjini Magharibi.

Alisema mtihani wa kuwapata washindi ulifanyika Agosti mwaka huu na washindi nane wanasakwa kuiwakilishi nchi kwenye mashindano ya hisabati ngazi ya Afrika Mashariki, Afrika na dunia.

Katibu Mkuu wa CHAHITA, Dk. Said Sima, alisema malengo yao mwakani ni kuhakikisha mikoa yote nchini inashiriki shindano hilo.

Alisema siyo kila mwanafunzi anashiriki bali ni wale wenye vipaji na wakuu wa shule ndiyo huwachagua wanafunzi wa kushiriki shindano hilo.

Naye, Mkuu wa Idara ya Hisabati Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Sylvester Rugeihyamu alisema lengo la shindano la hisabati ni kutambua na kuibua vipaji kwenye somo hilo, kuchochea na kutambua ubunifu wa uvumbuzi kupitia mitihani

Alitaja lengo lingine ni kuwapa motisha wanafunzi kupenda somo la hisabati.

# Serikali yaiagiza WCF kusajili waajiri wadogo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imeuagiza Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), kusajili kundi la waajiri wote wadogo kwa kuwa ndiko kwenye wafanyakazi wengi wanaopata madhara ikiwamo ulemavu wa kudumu na wengine kupoteza maisha kutokana na mazingira ya kazi.

Agizo hilo limetolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Mhandisi Cyprian Luhemeja, wakati akifungua kikao cha sita Baraza la pili la Wafanyakazi wa Mfuko wa WCF mjini hapa.

Mhandisi Luhemeja alisema licha ya Mfuko huo kusajili kwa kiwango kikubwa waajiri wakubwa na wa kati, lakini kipaumbele kinapaswa kuwekwa kwa waajiri wadogo kwakuwa kiwango kilichosajiliwa bado ni kidogo tofauti na uhalisia.

"Naagiza Mfuko huu wa WCF ifakapo Juni mwakani nipewe takwimu za usajili wa waajiri wadogo ambao ndio kwenye wafanyakazi wenye matatizo mengi kazini ikilinganishwa na waajiri wakubwa," alisema.

Alifafanua kuwa kwenye waajiri wadogo ndiko kwenye wafanyakazi wanaopata madhara wakiwa kazini ikiwamo kupata ulemavu wa kudumu na wengine kupoteza maisha kutokana na mazingira ya kazi yaliyokuwapo na kwamba ni lazima wapewe umuhimu.

"WCF mnapaswa kuvaa viatu vya ulemavu kwakuwa mfuko huo ni tofauti na mifuko mingine inayohudumia watu wenye afya njema ambao wafanyakazi wakiumia kazini mzigo huo wa kuhudumia mnaubeba nyinyi," alisema Luhemeja.

Aidha alitaka Mfuko huo kubuni vyanzo vya kuongeza mapato yatakayochangia kutoa mafao bora kwa wateja wao ili waweze kunufaika nao.

Aliagiza wajumbe wa Baraza hilo kuzipitia sheria ambazo zimepitwa na wakati ili kupendekeza kwenye vikao vya juu ili ziweze kufanyiwa marekebisho kulingana na mazingira ya sasa.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, alisema Mfuko utaendelea kuimarisha mifumo ya utendaji kazi ya usajili na watashirikiana na taasisi nyingine zenye kanzidata za waajiri ikiwamo BRELA, TRA, NSSF kwa kuhakikisha wanabadilisha taarifa.

Dk. Mduma alisema mpango huo wa kubadilishana taarifa utawasaidia waajiri wapya wanawa kwenye kanzidata ya mfuko ili kuwasajili na wale watakaoondoka katika biashara itakuwa ni rahisi kuwaondoa kwenye orodha ya usajili.

Kuhusu kuleta ubunifu wa mifumo ya ndani, alisema mifumo ya ndani inasomana na kuhakikisha kazi inaenda kwa kasi na kwamba mifumo hiyo inasomana na mifumo ya taasisi nyingine itasaidia kuboresha huduma za mfuko na kupunguza gharama za uendeshaji na kwa wateja hasa wanaodai fidia zao.

Alisema kwa sasa Mfuko umefikia asilimia zaidi ya 92 ya waajiri ambao wapo kwenye kanzidata, waajiri wakubwa wamesajiliwa asilimia 100, wa kati asilimia 92 na waajiri wadogo kulingana na mazingira yao usajili wao upo chini ya asilimia 90.


halotel

TAARIFA KWA UMMA

Viettel Tanzania PLC (Halotel) ni kampuni ya mawasiliano inayoendelea kuboresha huduma na kuvunja mipaka ya mawasiliano kwa wateja wetu kwa kutoa gharama nafuu kwenye SMS, Huduma za kupiga simu na Intaneti.

Tunapenda kuwatangazia wateja wetu na umma kwa ujumla juu ya gharama zetu za makato pindi mteja atakapokuwa hajajiunga kwenye kifurushi.

GHARAMA ZA NDANI YA NCHI

| Kipengele | Gharama |
|---|---|
| Kupiga Halotel kwenda Halotel | 10 Tsh/Dk |
| Kupiga Halotel kwenda mitandao mingine | 20 Tsh/Dk |
| Kutuma SMS | 5 Tsh/SMS |
| Data (MB) | 9.35 Tsh/MB |

GHARAMA ZA NJE YA NCHI

GHARAMA ZA KUPIGA SIMU NJE YA NCHI

| Kanda | Gharama (Tsh/Dk) |
|---|---|
| **Ukanda 1:** USA, UK, India, China, Canada, Australia, Japan, South Korea, Vietnam, Laos, Cambodia | 450 |
| **Ukanda 2:** Nchi nyingine za ULAYA, Kenya | 750 |
| **Ukanda 3:** Rwanda, Afrika Kusini, Zambia, UAE, Oman,Haiti, Peru | 840 |
| **Ukanda 4:** Cameroon, Zimbabwe, Malawi, Uganda, Congo DRC, Mozambique | 1,000 |
| **Ukanda 5:** Burundi | 1,350 |
| **Ukanda 6:** Sehemu nyingine duniani | 2,700 |
| **Ukanda 7:** Mitandao ya satelite | 13,800 |

GHARAMA ZA KUTUMA SMS NJE YA NCHI

| SMS | Gharama |
|---|---|
| SMS kwenda nje ya nchi | 95 Tsh/SMS |

| Aina ya kifurushi | Muda | Gharama (Tsh) | Mitadao Yote (Tsh) | Halotel-Halotel (Tsh) | SMS | Data (MB) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| VIFURUSHI VYA SAUTI | | | | | | |
| Sauti | Siku | 350 | 25 | | | |
| Sauti | Siku | 500 | | 110 | | |
| Sauti | Siku | 500 | 60 | | 60 | |
| Sauti | Siku | 500 | 60 | 60 | 60 | |
| Sauti | Siku | 1,000 | 180 | | 60 | |
| Sauti | Siku | 1,000 | 180 | 60 | 60 | |
| Sauti | Siku | 700 | 10 | Kila Dk 5 za mwanzo bure | | |
| Sauti | Wiki | 1,500 | 180 | | 150 | |
| Sauti | Wiki | 2,000 | 500 | | 300 | |
| Sauti | Wiki | 2,500 | 350 | 50 | 150 | |
| Sauti | Wiki | 3,000 | 450 | | 150 | |
| Sauti | Mwezi | 4,000 | 400 | 50 | 50 | |
| Sauti | Mwezi | 5,000 | 550 | | 100 | |
| Sauti | Mwezi | 5,000 | 300 | 1,200 | 100 | |
| Sauti | Mwezi | 10,000 | 1,600 | 1,600 | 150 | |
| Sauti | Bila Kikomo | 500 | 20 | | | |
| VIFURUSHI VYA SMS | | | | | | |
| SMS | Daily | 100 | | | 200 | |
| SMS | Weekly | 500 | | | 2000 | |
| SMS | Monthly | 1,000 | | | 10,000 | |
| VIFURUSHI VYA INTANETI | | | | | | |
| Intaneti | Siku | 350 | | | | 170 |
| Intaneti | Siku | 500 | | | | 245 |
| Intaneti | Siku | 1,000 | | | | 490 |
| Intaneti | Siku | 2,000 | | | | 985 |
| Intaneti | Siku 10 | 2,100 | | | | 1024 |
| Intaneti | Wiki | 1,000 | | | | 490 |
| Intaneti | Wiki | 2,000 | | | | 985 |
| Intaneti | Wiki | 3,000 | | | | 1475 |
| Intaneti | Wiki | 5,000 | | | | 2460 |
| Intaneti | Wiki | 10,000 | | | | 4925 |
| Intaneti | Mwezi | 10,000 | | | | 4920 |
| Intaneti | Mwezi | 20,000 | | | | 9850 |
| Intaneti | Mwezi | 30,000 | | | | 14780 |
| Intaneti | Mwezi | 50,000 | | | | 24600 |
| Intaneti | Bila Kikomo | 500 | | | | 200 |
| VIFURUSHI VYA COMBO | | | | | | |
| Unibang | Wiki | 1,500 | 5 | 25 | 5 | 700 |
| Unibang | Siku 14 | 3,000 | 50 | 50 | 25 | 1300 |
| Unibang | Mwezi | 10,000 | 50 | 250 | 50 | 4500 |
| Combo | Mwezi | 10,000 | 280 | | 50 | 4000 |
| Combo | Mwezi | 20,000 | 400 | | 100 | 8500 |
| Combo | Mwezi | 50,000 | 600 | | 200 | 22000 |

# 17,000 walamba ajira Jeshi la Polisi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, amesema zaidi ya askari 17,000 katika Jeshi la Polisi wameajiriwa na asilimia 80 ya askari wa jeshi hilo wamepandishwa vyeo katika kipindi cha miaka miwili na nusu.

Alibainisha hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara kuelezea mafanikio ya serikali ya sasa.

Masauni alisema kwa upande wa bajeti ya wizara hiyo, imeongezeka kwa zaidi ya asilimia 44 na kwamba Wakuu wa Polisi wa Wilaya, kila mmoja hivi sasa ana gari, hali iliyorahisisha utendaji kazi.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akizungumzia mafanikio ya mkoa huo wakati wa mkutano huo, alisema Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) awamu ya tatu umetoa mikopo ya ruzuku zaidi ya Sh. bilioni 15.8 kwa walengwa 57,012 wa mkoa huo katika kipindi cha kuanzia Machi hadi Septemba mwaka huu.

Alisema sekta ya afya imeimarika kwa kiasi kikubwa kwa kusogeza huduma kwa wananchi, miundombinu ya afya iliyojengwa na kukamilishwa imesaidia wananchi kuwa na uhakika wa kupata matibabu.

Alisema Sh. bilioni 51.572 zimetolewa na serikali kwa ajili kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwamo ujenzi wa hospitali nne mpya, ukarabati wa hospitali moja, ujenzi wa vituo vya afya 22 na ukamilishaji wa zahanati 69.

Pia ujenzi wa majengo matatu ya dharura (EMD), majengo mawili ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU) na ujenzi wa nyumba sita (3 in 1) za makazi za watumishi wa afya.

Fedha hizo pia zimetumika katika ununuzi wa vifaa tiba na dawa kwenye hospitali za wilaya saba, vituo vya afya 22 na zahanati 220, ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida na ukarabati wa hospitali kongwe za Manyoni na Iramba.

Kwa sekta ya elimu, katika kutekeleza Mpango wa Utoaji Elimsingi Bila Malipo, Sh. bilioni 61.105 zimetolewa katika kipindi cha miaka miwili.

Kutokana na fefha hizo, shughuli zilizotekelezwa ni ujenzi wa madarasa 814 katika shule shikizi na msingi, madarasa 38 ya awali na madarasa 617 katika shule za sekondari, ujenzi wa matundu 1,866 ya vyoo katika shule za msingi na matundu 328 katika shule sekondari.

Kazi nyingine iliyofanywa ni ukamilishaji wa maabara 85, ujenzi wa mabweni 48, mabwalo sita, nyumba za watumishi 65, majengo ya utawala 12, ujenzi wa shule mpya 16 za sekondari za kata pamoja na shule moja ya sekondari ya mkoa.

Serukamba alisema walimu 826 wameajiriwa Idara ya Elimu Msingi na walimu 427 katika Idara ya Elimu ya Sekondari.

Katika sekta za uzalishaji, alisema mkoa ulipokea fedha Sh. bilioni 44.386 kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambapo tani 2,973 za mbolea ya ruzuku zimesambazwa na kuwanufaisha wakulima 8,342 na tani 863.004 za mbegu za ruzuku za alizeti zilipokewa na kusambazwa.

Aliongeza kuwa kabla ya kupatiwa ruzuku ya mbolea kutoka serikalini, kiwango cha uzalishaji mazao ya kilimo kilikuwa tani 1,120,566 kwa mazao ya chakula, biashara, mboga na matunda kwa msimu wa 2021/22, lakini baada ya serikali kutoa ruzuku ya mbolea mwaka wa fedha 2022/23, uzalishaji umeongezeka kutoka tani 1,120,566 hadi 1,507,226.9 sawa na ongezeko la asilimia 74.3.



Alibainisha kuwa zao la alizeti kabla ya kutolewa ruzuku ya mbegu, uzalishaji wake ulikuwa tani 145,915.8 zilizolimwa mwaka 2021/22 na sasa umefikia tani 311,318.38 zilizolimwa katika mwaka 2022/23 baada ya serikali kutoa ruzuku ya mbegu.

Serukamba pia alisema maeneo 92 ya mkoa yametambuliwa kama maeneo muhimu ya umwagiliaji ambapo kati ya hayo, skimu zilizopo ni 38. Kati yake, skimu 19 zimeendelezwa, skimu 19 hazijaendelezwa na 54 ya maeneo yaliyobaki yamebainika kuwa yanafaa kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji ndani ya Mkoa wa Singida.


The United Republic of Tanzania
President's Office, State House

VACANCY ADVERTISEMENT

Tanzania Social Action Fund (TASAF) is currently implementing Productive Social Safety Net Program which aims at protecting the Vulnerable Poor Households from severest consequences of poverty by implementing interventions that will lead to increased Household incomes and opportunities while increasing consumption.

The Permanent Secretary, President's Office, State House is inviting applications from suitably qualified candidates to fill the vacant post of **TASAF Executive Director.**

Job Description and required qualifications for the post is available in TASAF website:- www.tasaf.go.tz

How to apply;

1) a) Applications, enclosing scanned certified copies of certificates and Curriculum Vitae be sent to the following address:-

Permanent Secretary, President's Office
Tanzania Social Action Fund (TASAF)
Kambarage Tower Building
Jakaya Mrisho Kikwete Road
P.O. Box 2719
**DODOMA.**

b) Applications (In PDF Format), enclosing scanned certified copies of certificates, birth certificate and Curriculum Vitae be sent through the following email address: hr@tasaf.go.tz

2) Applications made in a way other than the above will not be considered. Deadline for receiving applications is 10th November, 2023.

PERMANENT SECRETARY
PRESIDENT'S OFFICE, STATE HOUSE

217637802


## Bil. 1/- zatolewa kuwezesha mitaji ya wanawake, vijana

**Na Mwandishi Wetu,** NEWALA

KATIKA kuwafikia na kuwanufaisha zaidi wanawake wajasiriamali, CRDB Bank Foundation imeshiriki Mkutano Mkuu wa Nne wa Mwaka wa BUTA Vicoba uliowakutanisha zaidi ya wanachama 3,500 kutoka vikundi 318 vilivyoshiriki na kutoa mtaji wezeshi wa fedha taslimu na pikipiki.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Mwambapa, alisema kwa hamasa aliyoiona ameamini BUTA Vicoba ni taasisi kubwa yenye uwakilishi nchi nzima, jambo linaloleta matumaini ya kulikomboa kiuchumi kundi hilo.

Tully alisema ni jambo la kujivunia kuona wanawake wanakusanyika kwa pamoja kupanga maendeleo ya uchumi wao binafsi na wa familia zao, hivyo kuongeza ushiriki wao kwenye uchumi wa taifa.

"Leo (jana) tunakabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 20 pamoja na pikipiki tano zenye thamani ya Sh. milioni 15 kwa wana BUTA Vicoba. Huu ni mtaji wezeshi kwa baadhi yenu waliokidhi vigezo.

"Lengo la kuanzishwa kwa CDRB Bank Foundation ni kuwahudumia Watanzania hasa makundi yasiyopewa kipaumbele na taasisi nyingi za fedha nchini ambayo ni wanawake na vijana. Mliopata mtaji huu wezeshi leo, mnaungana na wenzenu ambao tayari tumeshatoa Sh. bilioni moja kwao," alisema Tully.

CRDB Bank Foudation ni kampuni tanzu ya Benki ya CRDB iliyoanzishwa na kusajiliwa mwaka 2022 kwa lengo mahsusi la kuwawezesha vijana na wanawake. Kwa sasa taasisi hii inatekeleza Programu ya Imbeju iliyotengewa bajeti ya kuanzia Sh. bilioni 5 kwa ajili ya makundi hayo.

Ili kuyafikia makundi hayo kirahisi, inashirikiana na wadau muhimu wenye mtandao mpana. Kwa vijana wenye ubunifu wa kiteknolojia (start-ups), taasisi inashirikiana na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Tume ya TEHAMA (ICTC) na kwa wanawake wajasiriamali kuna BUTA Vicoba, Shirika la Care International, Citizen Foundation na wengine.

Tangu Programu ya Imbeju ilipozinduliwa Machi 12 mwaka huu, vijana 709 walijitokeza kutuma maombi ambayo yalipochujwa, miradi 196 ilikubaliwa na kuingia hatua ya mafunzo ya kujengewa uwezo wa kuendesha biashara kwa viwango vinavyofaa ndani ya nchi na kimataifa.

Kazi za ubunifu 51 kati ya 196 zilikidhi vigezo vya kuendelea na tayari baadhi ya vijana wa kundi hili wameanza kupewa mtaji wezeshi ili kukuza miradi yao.

Kuhusu mafunzo ya ujasiriamali na elimu ya fedha, Tully alisema makundi yote mawili yanapata na mpaka sasa tayari zaidi ya wajasiriamali 100,000 wamefunzwa; wanawake kwa wanaume.

Tully pia aliitumia nafasi hiyo kumpongeza Mkurugenzi wa BUTA Vicoba, Semeni Gama kwa jinsi anavyojitoa kuhakikisha wananchi wanajikwamua kiuchumi.

Naye Semeni alishukuru Benki ya CRDB kupitia taasisi yake ya CRDB Bank Foundation kwa jinsi ilivyojitoa kuwawezesha wanawake ambao wengi hawapewi nafasi kwenye taasisi nyingi za fedha kutokana na kutokidhi vigezo vilivyowekwa.

"Ili kupata mkopo kwenye taasisi nyingi za fedha nchini, mteja anahitaji kuwa na dhamana, lakini wanawake wengi hawamiliki ardhi kutokana na mila zilizopo maeneo mengi. Programu ya Imbeju ambayo imeondoa kigezo hicho inawafaa wanawake wengi watakaoweza kuanzisha biashara zao, hivyo kujiingizia kipato cha uhakika," alisifu Semeni.



## Kamati ya Bunge yaagiza ajira zaidi TAEC

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), imeitaka serikali kutoa kibali cha ajira za watumishi wa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC), ili kuendana na uwekezaji mkubwa uliofanywa katika maabara ya kisasa iliyogharimu Sh.bilioni 10.4

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Agustine Vuma Holle, akizungumza mwishoni mwa wiki, jijini Arusha, alisema wameridhishwa na utekelezaji wa mradi huo lakini hawajaridhishwa na idadi ya watumishi walioko kazini.

"Kutokaa na uwekezaji huu mkubwa uliofanywa na serikali yetu, sisi kama kamati, tunaitaka serikali kuongeza watumishi zaidi ili kuendana na uwekezaji huu wa kisasa na wakohistoria,"alisema.

Alisema maabara hiyo nzuri inavifaa vya kisasa, hivyo vizuri wawepo watumishi wengi na wenye ujuzi wa kufanya kazi katika maabara hiyo ili lengo la serikali litimie la kuwa na maabara yenye tija kwa taifa na nje ya nchi.

Mkurugenzi wa TAEC, Prof. Lazaro Busagala, alisema ili kuwasogezea karibu wananchi huduma wameanzisha kanda saba, hawataishia kuwekeza katika Mkoa wa Arusha pekee.

Pia, aliomba kamati hiyo kuwasaidia TAEC kuiomba serikali, kuendelea kuwekeza kwenye kuongeza idadi ya watumishi pamoja na kuendeleza wataalamu wa mionzi, kwa kutenga fedha sambamba na kuweka mpango mkakati mzuri wa kuhakikisha wataalamu wanaongezeka kwa wingi.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Iadslaus Mnyole, alisema TAEC ina majukumu mbalimbali yakiwemo ya kufanya utafiti na bunifu kwenye eneo la teknolojia ya mionzi kwa sababu ina manufaa katika sekta mbalimbali nchini.

Mtafiti kutoka TAEC Kanda ya Kaskazini, Dennis Mwalongo, alisema moja ya kazi za tume hiyo ni kupima uchafuzi wa anga, unaotokana na majaribio ya silaha za nyuklia, kuendeleza teknolojia ya nyuklia katika kilimo.

# DCEA yanasa 69 tuhuma kulima bangi, mirungi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imesema katika kipindi cha Juni hadi Oktoba imewakamata watuhumiwa 69 wanaojihusisha na kilimo cha bangi katika mikoa mbalimbali.

Taarifa za kunaswa wananchi hao zilitolewa na Kamishna Jenerali wa Mamlaka hiyo, Aretas Lyimo wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kushiriki wiki ya vijana kitaifa na kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru.

Lyimo alisema wamejipanga kufanya operesheni mikoa yote na kutoa elimu kwa kuwa mikoa yote inalima bangi na mirungi.

Aidha, alisema kwa operesheni ambazo wameishafanya Arusha walikamata watu 19, Kilimanjaro (11), Morogoro (19), Iringa tisa, Mara (11) na mikoa ya Dar es salaam na Pwani hakutaja idadi licha ya operesheni kufika.

Aliongeza kuwa watazishirikisha mamlaka za maji na mabonde kwa kuwa wananchi wanalima dawa za kulevya kwenye vyanzo vya maji.

Alisema awali walipoanza operesheni walianza na dawa za kulevya za viwandani zikiwemo heroine na cocaine ila walifanikiwa kuzidhibiti kwa kiasi kikubwa.

Vile vile alisema baada ya mamlaka hiyo kufanikiwa kudhibiti matumizi ya dawa za viwandani sasa watu wengi wamegeukia matumizi ta bangi na mirungi.

Lyimo alisema watahakikisha tatizo la dawa linaisha katika jamii ili kila mtu apate kipato chake halali kisicho cha kulima au kutumia bangi na mirungi na kuharibu ubongo.

Pia, alisema madhara ya kutumia bangi na mirungi hayaishii kwa watumiaji tu bali yanawafikia watu wengine ndiyo maana wanataka watokomeze uuzaji wa dawa kwa asilimia 80.

Alisema sheria inakataza kilimo cha bangi na mirungi, mtu anayebainika kuilima adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 au kifungo cha maisha jela.

Akitoa ufafanuzi wa kwa nini kilimo cha bangi kisiruhusiwe kama zifanyavyo nchi zingine, alisema bangi inayolimwa nchini ni tofauti na ile ya mataifa mengine kwamba inalimwa kwa ajili ya dawa, lakini ya Tanzania inaharibu ubongo.



Mchimbaji maarufu wa madini ya Tanzanite, Bilionea Saniniu Laizer (katikati) akizungumza baada ya kuongoza harambee ya ujenzi wa uzio wa Shule ya Msingi Naisinyai wilayani Simanjiro Mkoani Manyara, iliyoanzishwa mwaka 1974 na kupatikana shilingi milioni 38.6, jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# KINAPA yaongeza milango washiriki miaka 62 ya Uhuru

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

IDADI kubwa ya watu waliotia nia ya kuongozana na wazalendo, watakaoipandisha bendera ya taifa katika kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro, Desemba 3 mwaka huu, imeisukuma Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA), kuongeza malango mawili zaidi, yatakayotumiwa kunogesha maadhimisho ya miaka 62 ya uhuru.

Bendera hiyo itasimikwa na wazalendo hao kwa msimu wa tatu mfululizo kwenye kilele cha uhuru, chenye urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari.

Akizungumza jana katika lango la Marangu, Wilaya ya Moshi, ambako kulifanyika uzinduzi wa kampeni ya uhamasishaji, Ofisa Utalii wa hifadhi hiyo, Vitus Mgaya, alisema Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), limeguswa na kazi inayotarajiwa kufanyika na limeelekeza kuongezwa kwa malango mawili ya Machame na Lemosho, badala ya kutegemea lango la Marangu pekee.

"Huu ni msimu wa tatu wa kampeni ya kusimika bendera juu ya Mlima Kilimanjaro. Tumeongeza gate (lango) la Machame lililoko Wilaya ya Hai na Lemosho Gate, lililoko Wilaya ya Siha, na sasa tutakuwa na njia tatu pamoja na ile ya Marangu (Wilaya ya Moshi)," alisema.

Aidha, alisema katika msimu huu wanatarajia pia kuongeza mawakala wa kupandisha wageni katika mlima huo ili kutoa fursa zaidi kwa washiriki.

Akifafanua zaidi kuhusu kampeni hiyo, Ofisa hifadhi Mwandamizi wa KINAPA, Stephan Moshi alisema: "Tunahama katika kutegemea utali wa nje, tunahamia katika soko la ndani ili kuboresha mapato yetu kama nchi na kujenga uzalendo kwa Watanzania kuhusu rasilimali na vivutio vyao vya utalii.

Aidha, baadhi ya mawakala wanaotarajia kupandisha wazalendo hao, akiwemo Simbo Natai, ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya African Scenic Safari, alisema wao kwa siku nane watatoza gharama ya mtu mmoja Sh. 1, 700,000.

# Vijiji 20 vyachukua hatua kujinusuru kuwa jangwa

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

VIJIJI 20 vya wilaya za Korogwe na Handeni mkoani Tanga, vilivyokuwa tishio kwa uharibifu wa mazingira vimechukua hatua ya kunusuru eneo hilo kugeuka jangwa. Hatua hiyo imekuja baada ya vijana 1,000 kujitosa kutoa elimu ya kukabiliana na mabadiliko hayo ya tabianchi.

Eneo hilo lilikuwa limeathiriwa kwa kiasi kikubwa na ukame kutokana kukithiri kwa kilimo kisicho na tija, ufugaji na shughuli nyingine za binadamu.


Akizungumza mwishoni mwa wiki, jijini Arusha katika hafla ya kufunga mradi wa sauti ya vijana, Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Antos Silayo, alisema kama vijana wasipochukua hatua sasa, wakaishi maisha mazuri na mazingira yakasapoti vizazi vyao vya mbeleni, hakutakuwa na taifa.

Mradi huo wa uhahamasishaji wa utunzaji mazingira (sauti ya vijana) katika wilaya hizo, unatekelezwa na Shirika la World Vision Tanzania (WVT) na Umoja wa Ulaya.

Mratibu wa Mradi wa Sauti ya Vijana wa WVT, Shukrani Dickson, akizungumzia mradi huo, alisema alisema umetekelezwa kwa mafanikio katika wilaya hizo mbili kwa miaka mitatu, kuanzia mwaka 2020. "Ili kuhilili mabadiliko ya tabianchi na kukabiliana na mabadiliko hayo, vijana hao wametoa elimu kwa wananchi wasilime karibu na vyanzo vya maji, umbali wa mita 60.

"Tumewafikia wananchi 24,000 katika wilaya zote mbili za Korogwe na Handeni. Tumesaidia kampeni ya upandaji miti ya kitaifa, kwa kila wilaya kupanda miti, laki moja na elfu moja mia saba; na katika hiyo miti ambayo tumepanda, nusu ya hiyo miti ni ya matunda"alisema.

Katika mkutano huo, Kaimu Ofisa Mipango, Mkoa wa Tanga, Athanas Michael, alisema serikali imeridhishwa na vijana wengi katika mkoa huo, kupata elimu hiyo, kuwezeshwa kufikia ndoto zao za kiuchumi na kuakisi moja kwa moja maono ya Rais, Samia Suluhu Hassan katika Programu ya Building Better Tomorrow (BBT).



# TPA yawatangazia neema w'biashara Kanda ya Ziwa

**Na Vitus Audax,**
MWANZA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Nchini (TPA) Kanda ya Ziwa Victoria imewatangazia wafanyabiashara na wadau wa usafirishaji ndani na nje ya nchi ongezeko la fursa na ufanisi kiutendaji na kimiundombinu katika bandari hizo.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Meneja wa TPA Kanda ya Ziwa Victoria, Erasto Lugenge baada ya mazungumzo maalumu na wadau wa Bandari Kanda ya Ziwa.

Alisema mamlaka hiyo imeweka mikakati mahususi ya ushirikiano wa karibu na watendaji kutoka sekta zote zinazofanya kazi katika bandari zake kuhakikisha huduma zinatolewa haraka na kuongeza tija kwa wafanyabiashara wanaotumia bandari hizo.

"Tunawahakikishia wateja wetu kuwa TPA imejipanga kuwahudumia vyema kwani tumeboresha miundombinu pamoja na vitendea kazi na tayari maeneo mengine tunaendelea na ukarabati na matengenezo makubwa kuhakikisha wateja wetu wanapata huduma stahiki," alisema Wakili Lugenge.

Aidha, alisema katika kuhakikisha mamlaka hiyo inaongeza shehena katika usafirishaji nje ya nchi kwa sasa wamekuwa na mawasiliano na kampuni za nje ikiwa ni pamoja na Uganda kuongeza shehena ya usafirishaji wa makaa yam awe.

Aidha, alisema kuwa kama watoa huduma bandarini wameadhimia kwa pamoja kutoa huduma kwa mawasiliano ya karibu zaidi ili kuhakikisha mteja anapoingiza mzigo bandarini taasisi zote zihakikishe zinatoa huduma kwa wakati.

Kuhusu uboreshaji miundombinu bandarini alisema kuwa serikali imeweka mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miradi mikubwa katika Bandari za Ziwa Victoria inayoenda sambamba na upanuzi pamoja na ujenzi wa miundombinu.

Mwakilishi wa kampuni ya usafirishaji wa makaa ya mawe ya Ziwa Maisha kutoka Uganda, Robert Mushi, alisema kama wasafiri wakuu katika bandari hizo wanafurahishwa na utendaji kazi katika bandari hizo kutokana na huduma kuboreshwa zaidi.

Alisema kwa sasa wanahitaji kuongezewa meli yenye uwezo wa kusafirisha tani nyingi zaidi kwa sababu mizigo ipo ya kutosha lakini meli inayosafirisha mizigo hiyo kwenda Uganda ni moja.



Baadhi ya Wataalamu kutoka Halmashauri za wilaya za Msalala na Nyang'hwale wakifuatilia mada wakati wa mafunzo ya kanuni mpya za wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii za mwaka 2023 (CSR) (The Mining- Corporate Social Responsibility 2023) yaliyoandaliwa na Mgodi wa Barrick Bulyanhulu kwa kushirikiana na Tume ya Madini yaliyofanyika mgodini hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi walia kubambikizwa bili, waomba mita za Luku

**Na Shaban Njia,**
KAHAMA

WAKAZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wameiomba Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA) kuwafungia mita za Luku kama ilivyo kwa TANESCO ili kuondoa malalamiko ya ongezeko la bili za maji.

Diwani wa Kata ya Kahama Mjini, Hamidu Juma, aliwasilisha ombi hilo kwa niaba ya wananchi wakati wa kikao cha kawaida cha baraza la madiwani la halmashauri hiyo cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24. Alisema malalamiko ya wananchi yamekuwa mengi juu ya uwepo wa bili kubwa za maji.

Hamidu alisema ili kuondoa malalamiko hayo ni vema KUWASA ikaja na utaratibu mpya wa kuwafungia wateja wake mita za Luku za maji ambazo mteja atakuwa analipia kabla ya matumizi.

Alisema maofisa wa KUWASA wamekuwa wakisoma mita za maji bila kushirikisha wamiliki wa makazi ili watambue kwa mwezi ametumia kiasi gani.

"Shirikia la Umeme Tanzania (TANESCO) linautaratibu wa mita za Luku ya kulipia kiwango cha matumizi na hakuna mteja anayelalamika, hii ingetakiwa kuwa kwenye mamlaka yetu ya maji KUWASA ingeondoa malalamiko haya tumechoka kukutana na wananchi na kuwafafanulia juu ya hili" alisema.

Diwani wa Nyasubi, Abel Shija alisema, mita za luku za maji ndio suruhu ya kumaliza malalamiko ya wananchi juu ya ongezeko la bili za maji kila mwezi.

Akijibu hoja hiyo, Ofisa Uhusiano wa KUWASA, John Mkama alikili kuwepo kwa malalamiko hayo kwa baadhi ya wateja wao akisema wanapofika kusoma mita wanawashirikisha mteja ili kutambua kiwango alichotumia kabla ya kumtumia kwenye simu na kufanya malipo.

Alisema TANESCO wamekuwa kiteknolojia, ndio maana hakuna malalamiko kwa sababu walianza majaribio kwa mita 25 za Luku, hawakupata matokea mazuri.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Yahya Bundala aliwashauri KUWASA kujipanga upya na mfumo wa Luku za maji kwa kurekebisha pale walipogudua kunamakosa.

## Wanafunzi waomba serikali, Azaki kudhibiti ukatili

**Na Timothy Itembe,** TARIME

SERIKALI imeombwa kushirikiana na asasi zisizokuwa za kiserikali kwa lengo la kutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia husasani kwa watoto wa kike ili watimize ndoto zao.

Hayo yanabainshwa na wanafunzi wakati asasi ya Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF) kwa kushirikiana na Halamashauri ya Wilaya ya Tarime walipotoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi ili kuhakikisha wasichana wanapata haki zao za msingi.

Machere Chuma ni mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Manga alisema kuwa elimu iliyotolewa katika maadhimisho hayo iwe endelevu kwa lengo la kubadili mitazamo hasi kwenye jamii ambayo bado inaendeleza suala la ukatili.

Janeth Marwa ambaye pia ni mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Manga alisema jamii haina budi kuendelea kuthamini mtoto wa kike kwa kupewa haki zake za msingi bila kusahau elimu, mahitaji muhumu pamoja na malezi bora ili aweze kutimiza ndoto zake.

Ofisa Miradi kutoka CDF Tarime, Anold Massawe alisema wameamua kuungana na serikali kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii ili kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia ili kuhakikisha mtoto wa kike anapata haki zake.

## Serikali yajipanga kutokomeza utumikishwaji watoto

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imejipanga kutokomeza vitendo vya utumikishwaji wa watoto katika mashamba na kujenga mazingira ya upatikanaji wa kazi zenye staha.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na wenye Ulemavu), Profesa Joyce Ndalichako, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizindua mradi wa kazi zenye staha katika sekta ya pamba nchini.

Alisema mradi huo utatekelezwa kwa miezi 24 kati ya Serikali ya Tanzania, Brazil na Shirika la Kazi Duniani (ILO) ambao utagharimu Dola za Marekani 558,170 (Sh.bilioni 1.39), ukilenga kukuza kazi za staha katika mnyororo wa thamani wa uzalishaji wa pamba na kulinda haki za watoto.

Alisema serikali imeweka mikakati ya kutokomeza utumikishwaji wa watoto ikiwemo kusaidia uanzishwaji wa Mpango Kazi wa Taifa dhidi ya Utumikishwaji wa Mtoto.

"Kuna mkakati wa uzingatiaji wa viwango vya kazi katika mnyororo wa thamani za zao la pamba na kukuza viwango vya usalama na afya katika mnyororo wa thamani," alisema.

Alisema pia kuna kuongeza kwa wigo wa kinga jamii katika maeneo ya kilimo cha pamba na kuimarisha uzalishaji wa pamba bora yenye thamani katika soko la dunia.

Alisema mradi huo utaleta manufaa kwa wananchi na wakulima wa pamba hasa kupata elimu ya madhara ya uvunjaji wa haki za watoto katika utumikishwaji.

Mkurugenzi wa ILO, Kanda ya Afrika Mashariki, Jealous Chirove alisema Tanzania inakabiliwa na changamoto ya kutokomeza utumikishwaji wa watoto.

"Leo tumekutana na kuzindua mradi unaoashiria azimio letu la pamoja la kuvunja mzunguko huu wa utumikishwaji wa watoto, umaskini na ukosefu wa usawa," alisema.

Naye Balozi wa Brazil nchini, Gustavo Nogueira, alisema mradi huo utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya nchi hizo mbili kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi.

Nipashe
Spotika



WANASOKA WA5 WENYE REKODI NYINGI ZA DUNIA ZA GUINNESS 12 - 13







# MASHOTO WA5 BORA ZAIDI EPL

**LONDON, England**

WACHEZAJI wanaotumia mguu wa kushoto wana umuhimu mkubwa katika ulimwengu wa soka. Wanaongeza aina na kutotabirika kwa mashambulizi ya timu. Soka ni mchezo unaotawaliwa na wachezaji wanaotumia mguu wa kulia na wale wanaotumia mguu wa kushoto hutoa faida ya asili.

Wanapiga mpira kwa njia tofauti, huunda pembe tofauti na hutoa mtazamo mpya kwenye uwanja. Katika historia ya Ligi Kuu England, (PL) kumekuwa na wachezaji kadhaa maarufu wanaotumia mguu wa kushoto ambao wameacha alama isiyofutika kwenye mchezo huo.

Baadhi ya mifano ya wachezaji wanaotumia mguu wa kushoto ambao wamekuwa na ufanisi mkubwa kwenye ligi hiyo ni pamoja na Ryan Giggs, David Silva, Gareth Bale, Robin van Persie na Ashley Cole.

Makala haya yanawaangalia wachezaji watano bora wanaotumia mguu wa kushoto kwenye Ligi Kuu England kwa sasa...

#5 Pedro Neto | Wolverhampton

Pedro Neto amekuwa akicheza kwa staili ya aina yake katika hatua za mwanzo za msimu mpya wa Ligi Kuu. Ikiwa ameanza vizuri kuna uwezekano wa kubaki Wolverhampton Wanderers kwa muda mrefu.

Mshambuliaji huyo wa Ureno amekuwa na uwezo mkubwa kiasi kwamba ana uwezekano wa kunyakuliwa na mmoja wa wababe wa Ulaya msimu ujao wa majira ya joto. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amesababisha maumivu ya kichwa kwa wapinzani kwa ustadi wake mzuri wa kucheza chenga na uwezo wa kupiga mipira ya hatari ndani ya eneo la hatari.

Amefunga bao moja na kutoa asisti tano katika mechi nane za Ligi Kuu hadi sasa msimu huu.

**#4 Martin Odegaard | Arsenal**

Nahodha wa Arsenal, Martin Odegaard, ni mmoja wa wachezaji bora kabisa kwenye Ligi Kuu England hivi sasa. Uchezaji wake wa miguu mahiri, ustadi mzuri wa kupiga pasi na humwezesha kusababisha maafa kwa timu pinzani na amekuwa na wakati mzuri zaidi kwa 'Washikabunduki' hao.

Si tu kwamba Odegaard ana uwezo wa kutengeneza nafasi za mabao kwa wachezaji wenzake, lakini pia anachangia kwa mabao mengi kutoka safu ya kiungo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amefunga mabao manne na kutoa asisti moja katika mechi 12 kwenye michuano yote aliyoichezea Arsenal hadi sasa msimu huu.

#3 Bukayo Saka | Arsenal

Katika msimu michache iliyopita, Bukayo Saka amejiimarisha kama mmoja wa mawinga bora zaidi duniani. Mshambuliaji huyo mahiri na asiyetabirika wa Arsenal ana ustadi mzuri na amekuwa muhimu zaidi kwa klabu na nchi katika siku za hivi karibuni.

Ana ustadi mzuri wa kuteleza na kutengeneza mashabulizi na amekuwa na jukumu muhimu katika ufufuo wa Arsenal chini ya Mikel Arteta.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amefunga mabao matano na kutoa pasi tano za mabao katika mechi 10 alizocheza kwenye mashindano yote hadi sasa msimu huu.

**#2 Mohamed Salah | Liverpool**

Mohamed Salah amekuwa muhimu kwa mafanikio ya Liverpool chini ya kocha Jurgen Klopp, siku za hivi karibuni. Mshambuliaji huyo raia wa Misri alijiunga na 'Wekundu' hao msimu wa majira ya joto wa 2017 na tangu wakati huo ameendelea kujitambulisha kama mmoja wa wachezaji bora zaidi wa enzi ya ligi.

Salah anajivunia kasi ya ajabu, pasi za ajabu na uwezo wa ajabu wa kufumania nyavu kutoka kwenye nafasi ngumu. Yote haya yanamaanisha kuwa amekuwa mmoja wa washambuliaji wa kufurahisha zaidi kuwatazama.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amefunga mabao nane na kutoa pasi nne za mabao katika mechi 11 katika michuano yote aliyoitumikia Liverpool hadi sasa msimu huu.

**#1 Erling Haaland | Manchester City**


Ukweli ni kwamba Erling Haaland anampa Lionel Messi ushindani katika mbio za Ballon d'Or 2023 inapaswa kutosha kuhalalisha nafasi yake juu ya orodha hii. Mshambuliaji huyo wa Norway alitwaa ubingwa wa Ligi Kuu England baada ya kujiunga na Manchester City msimu wa majira ya joto wa 2022.

Uwezo wake mkubwa wa kufunga mabao ukisaidiwa na mwendo wake wa akili, riadha na umaliziaji mzuri uliwapa City makali dhidi ya wapinzani wao waliposhinda mataji matatu ya kihistoria msimu uliopita.

Haaland amefanya kufunga mabao kuonekana rahisi na ana nafasi ya kushinda tuzo nyingi za Ballon d'Or katika siku zijazo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amefunga mabao tisa na kutoa pasi mbili za mabao katika mechi 13 alizocheza kwenye mashindano yote akiwa na Manchester City hadi sasa msimu huu.

## ISIKUPITE

Robert Lewandowski hadi sasa ndiye anayeshikilia rekodi ya Guinness ya kufunga mabao matano ndani ya dakika tisa, alifanya hivyo kwenye mechi ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, dhidi ya Wolfsburg mwaka 2015.



Extra Time



# WANASOKA WA5 WENYE REKODI NYINGI ZA DUNIA ZA GUINNESS

**LONDON, England**

KATIKA kiwango cha juu, wanasoka wanajulikana kwa uwezo wao wa kufanya mambo ya ajabu. Iwe ni kufunga mabao ya kustaajabisha au kuonesha ufundi wa hali ya juu.

Mafanikio haya ya ajabu mara nyingi husababisha wachezaji kuvunja rekodi na kuandika majina yao katika kurasa za hadithi za kitabu cha rekodi za dunia cha Guinness.

Iwe ni kuvuka idadi kubwa zaidi ya mabao yaliyofungwa katika msimu mmoja au kupata ushindi mwingi mfululizo, wachezaji hawa wanaacha alama isiyofutika kwenye historia ya mchezo huo wa soka.

Makala haya inawaangalia wanasoka watano wenye rekodi nyingi za Dunia za Guinness, twende sasa...

**#5 Ederson Moraes - rekodi 1 ya Guinness**

Ederson Moraes ni mmoja wa makipa bora zaidi duniani kwa sasa. Mlinda mlango huyo wa Manchester City ni kipa wa kisasa ambaye, pamoja na kuwa hodari katika kupiga mashuti na kutoa pasi za asisti, pia ni mzuri sana akiwa na mpira miguuni mwake.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil ana rekodi moja ya Dunia ya Guinness kwa jina lake. Anashikilia rekodi ya kupiga mkwaju mrefu zaidi wa mpira wa miguu (mita 75.45), ambao alifanya hivyo katika Kampasi ya Etihad pale Manchester Mei 2018.

Ederson anasifika kwa ustadi wake bora wa kusambaza mpira na uwezo wake wa kupiga mpira hadi ndani ya eneo la adui.

**#4 Neymar - rekodi 2 za Guinness**

Neymar ni mmoja wa wanasoka maarufu kwenye sayari hii. Raia huyo wa Brazil amewashangaza kwa uwezo wake wa hali ya juu na ufundi wa kucheza chenga za maudhi kwenye uwanja wa soka. Yeye bila shaka ni mmoja wa washambuliaji bora wa zama za kisasa.

Neymar ana rekodi mbili za dunia za Guinness kwa jina lake. Paris Saint-Germain ilimsajili kutoka Barcelona msimu wa majira ya joto wa mwaka 2018 kwa ada ya euro milioni 222, na kumfanya kuwa usajili ghali zaidi katika historia ya soka.

Neymar pia anashikilia rekodi ya bao la haraka zaidi kuwahi kufunga kwenye michezo ya Olimpiki. Aliweka mpira wavuni sekunde 14 pekee katika nusu fainali ya Brazil dhidi ya Honduras kwenye Michezo ya Olimpiki ya mwaka 2016.

**#3 Robert Lewandowski - rekodi 4 za Guinness**

Robert Lewandowski ni mmoja wa washambuliaji wakubwa wa kizazi chake. Katika miaka ya hivi karibuni, Lewandowski amevunja rekodi nyingi za ufungaji na ni mmoja wa wanamichezo hodari zaidi katika ulimwengu wa soka.

Mchezaji huyo wa Poland ana rekodi nne za Guinness kwa jina lake. Katika mechi ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, dhidi ya Wolfsburg mwaka 2015, Lewandowski alifunga mabao matano ndani ya dakika tisa baada ya kuingia kama mchezaji wa akiba. Kwa kufanya hivyo, alivunja rekodi nne.

Sasa anashikilia rekodi ya kufunga hat-trick ya haraka zaidi (dakika 3 na sekunde 22), kufunga mabao manne (dakika 6) na kufunga mabao matano. Lewandowski pia alivunja rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi akitokea benchi katika mechi hiyo hiyo.

**#2 Lionel Messi - rekodi 7 za Guinness**

Lionel Messi bila shaka ndiye mwanasoka mwenye vipaji zaidi wa kizazi chake (continued below)

Messi anashikilia rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufikisha mabao 50 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Alifanikisha hilo mnamo Aprili 2012 akiwa na umri wa miaka 24. Messi amekuwa kwenye 'gemu' 10 za michezo ya video, idadi ambayo ni kubwa zaidi ya mwanasoka yeyote duniani na anaingiza dola milioni 107 kwa mwaka.

Mwaka 2012, Messi alifunga mabao matano kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayer Leverkusen na kuwa mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi katika mechi moja kwenye mashindano hayo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, alitumia muda mwingi wa uchezaji wake Barcelona na anashikilia rekodi ya kucheza mara nyingi zaidi kwenye LaLiga akiwa mchezaji wa kigeni (mechi 520).

Wakati akiifungua Argentina hat-trick baada ya kuingia akitokea benchi katika mchezo dhidi ya Panama Juni 2016, Messi alivunja rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi kwenye mchezo wa Copa America akitokea benchi.

**#1 Cristiano Ronaldo - rekodi 16 za Guinness**

Cristiano Ronaldo ana rekodi 16 za Guinness na ni ushahidi wa kielelezo kamili cha binadamu ambacho amethibitisha kuwa. Ronaldo ndiye mfungaji bora wa kimataifa wa muda wote. Pia ndiye mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya (140).

Ronaldo alifunga mabao 17 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2013-14, mabao mengi zaidi ya mchezaji yeyote katika kampeni moja kwenye mashindano hayo. Anashiriki rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi katika msimu mmoja wa mashindano ya Uefa na Radamel Falcao, ambaye aliifungia Porto mara 17 kwenye Ligi ya Europa msimu wa 2011-12.

Ronaldo alifunga katika mechi 11 mfululizo za Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya misimu ya 2016-17 na 2017-18, rekodi ambayo haijavunjwa hadi leo. Pia ndiye mchezaji aliyefunga mabao mengi katika mashindano yote ya Klabu ya UEFA.

Kwa kufunga hat-trick katika mchezo wa ufunguzi wa Kombe la Dunia la FIFA 2018 dhidi ya Hispania, aliweka rekodi ya mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kufunga hat-trick kwenye Kombe la Dunia akiwa na miaka 33 na siku 130.

Ronaldo ndiye mchezaji pekee aliyefunga mabao matano katika Kombe la Dunia la FIFA akiwapita Uwe Seeler wa Ujerumani Magharibi, gwiji wa Brazil Pele na Mjerumani Miroslav Klose.

Gwiji huyo wa Ureno pia anashikilia rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi kwenye michuano ya euro (14) baada ya kumpita Michel Platini kwenye euro 2020.

Ronaldo anasifika kwa kutegemewa kwa mikwaju ya penalti na ndiye mfungaji wa penalti aliyefanikiwa zaidi katika historia ya LaLiga (72). Kwa mujibu wa tovuti ya Guinness World Records, alikuwa na alama asilimia 99 katika timu ya mwaka ya EA Sports FIFA 18, kiwango cha juu zaidi cha mchezaji yeyote kuwahi kutokea.

Ronaldo ndiye mwanamichezo anayefuatiliwa zaidi duniani kwenye Twitter, Facebook na Instagram. Ukurasa wa Wikipedia wa Ronaldo umekuwa na wageni zaidi ya trilioni 48 na anashikilia rekodi ya ukurasa uliotazamwa zaidi kwenye tovuti kwa mwanamichezo wa kiume.

Hivi karibuni alivunja rekodi ya mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi kwa wanaume katika soka la kimataifa alipocheza mechi yake ya 200 katika Timu ya Taifa ya Ureno katika mechi ya kufuzu kwa euro 2024 dhidi ya Iceland Juni 20, 2023.

## Nukuu


"Baadhi ya wachezaji wamekuwa wazi kila wanachotaka kukifanya. Wengine hawana uhakika na wengine wanataka kuona mambo yanavyoendelea. Nafikiri kitu kama hiki kipo kwenye kesi ya Eddie. Hatuwezi kukata tamaa kumshawishi ili aje Ghana. Lakini, hilo linategemea na mchezaji kile ambacho anataka," **Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa Ghana, Chris Huhton, akionesha kutokata tamaa kumshawishi mshambuliaji wa Arsenal, Eddie Nketiah, aache kuichezea England na kuhamia Ghana. Nyota huyo ambaye alizaliwa England, wazazi wake ni raia wa Ghana**



"Ninajaribu kuzungumza naye (Onana), kuhusu jinsi inavyokuwa Manchester United, kile unachopaswa kuchukua. Chochote ulichokifanya ni lazima ukiweke kwenye boksi moja kwa moja na uweke pembeni. Kwa hiyo ukikosea kwenye mchezo, inaweza kuwa kosa tunaloliona, linaweza kuwa kosa ambalo hatufanyi," **Kipa maarufu wa zamani wa United, Peter Schmeichel, akieleza namna anavyompa ushauri mlinda mlango wa klabu hiyo, Andre Onana**



"Si rahisi kwa mchezaji yeyote wakati hachezi kama anavyotaka. Lakini njia pekee ya kufanya hivyo ni kufanya kazi kwa bidii zaidi, kuonesha ari uliyonayo kwenye mchezo, kutoa mchango kwa timu kwa namna tofauti na unapopata nafasi jitahidi na ujaribu kuisaidia timu kushinda mchezo," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, akikiri haitakuwa rahisi kwa kipa Aaron Ramsdale kuishinda nafasi yake na namna anavyoweza kumpiku David Raya katika kikosi hicho.**



Nipashe
Spotika





Kiungo mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis, akiachia shuti katikati ya wachezaji wa Al Ahly, kwenye mechi ya African Football League iliyopigwa Ijumaa iliyopita katika Uwanja wa Mkapa na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2.

# WACHEZAJI WA5 SIMBA WALIOUPIGA MWINGI AFL

**Na Adam Fungamwango**

MARA ya mwisho Al Ahly kuruhusu zaidi ya bao moja kwenye wavu wake ilikuwa ni Machi 11, mwaka huu, ilipochapwa mabao 5-2, dhidi Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini katika mechi ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita ambao mwisho wa siku ilikwenda kutwaa ubingwa.

Baada ya hapo imecheza mechi 35 za Ligi ya Mabingwa msimu uliopita hatua ya makundi, Ligi Kuu msimu uliopita na huu, Kombe FA la Misri na Ligi ya Mabingwa hatua ya raundi ya kwanza bila kuruhusu wavu wake kufungwa mabao mawili, pamoja na kupoteza mechi yoyote ile.

Pamoja na hayo, Mabingwa wa Afrika, Al Ahly, Ijumaa iliyopita ilikutana na Simba katika mechi ya ufunguzi wa michuano ya African Football League kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na kuruhusu mabao mawili kwenye wavu wake, ikishindwa kulinda rekodi yake kwenye mechi ya 36.

Ilichofanikiwa kulinda ni kutopoteza kwani katika mechi zote hizo nyingi ilishinda na chache kutoka sare. Ilikuwa ni mechi ya aina yake, ikitawaliwa na ufundi mwingi, maarifa iliyofanana kabisa na hadhi ya michuano yenyewe.

Pande zote zilifanya mashambulizi na kukosa mabao ya wazi, lakini pia zikifanya makosa ya hapa na pale na mwisho wa siku timu hizo zikatoshana nguvu ya mabao 2-2, sasa ikisubiriwa mechi ya kesho nchini Misri ambayo ndiyo itaamua timu itakayosonga mbele.

Katika mechi hiyo, timu hizo ziligawana vipindi, Al Ahly ikitawala zaidi kipindi cha kwanza, kabla ya Simba kuzinduka kipindi cha pili na kama si kuzubaa kwa wachezaji wake kukaba nafasi na kuendelea kubishana na mwamuzi wakati wa faulo, ingeweza kuibuka na ushindi.

Katika makala haya tunawachambua wachezaji watano wa Simba ambao waling'ara kwenye mechi hiyo iliyohudhuriwa na watu mbalimbali mashuhuri kama Rais wa Shirikisho la Soka duniani (FIFA), Gianni Infantino, Rais wa Shirikisho la Mpira wa miguu barani Afrika (CAF), Patrice Motsepe, Kocha Mkuu wa zamani wa Klabu ya Arsenal, Arsene Wenger, mwamuzi maarufu za zamani wa kimataifa wa FIFA, Pierluigi Collina, Rais wa Heshima wa Simba, Mohamed Dewji na wengineo, wakiongozwa na Rais wa Zanzibar, Hussein Mwinyi.

# Kibu Denis

Kibu ameendelea kuwathibitishia mashabiki wa soka Tanzania kuwa si mchezaji wa majukwaa kama ambavyo wengi wanapenda wote wawe.

Makocha wote nchini, wawe wa Simba au Taifa Stars wamekuwa wakimpenda mchezaji huyo na kusema hadharani kuwa ni mmoja wa wachezaji bora kabisa nchini, lakini mashabiki mara kwa mara wamekuwa hawaelewi.

Kocha wa Simba, Roberto Oliveira, alipotua tu kwenye klabu hiyo, alimtaja kuwa ni mchezaji wa kwanza bora kumuona, akampa na zawadi kitu ambacho kwa mashabiki ilikuwa kama kichekesho.

Lakini baada ya hapo taratibu Kibu amekuwa akikata vidomodomo vya mashabiki ambao hawamkubali kwa sababu tu hana mbwembwe, chenga za maudhi ya visingino.

Katika mechi ya Ijumaa, aliendele kuthibitisha kuwa anaweza kukunyima vitu kadhaa uwanjani, lakini si maelekezo ya kocha, kukaba kuanzia juu, kuuficha mpira, kuwajibika, kujituma na kupambana.

Aliwaweka mabeki wa Al Ahly bize muda wote, na hata bao la kusawazisha alilofunga si kila mchezaji anaweza kufanya hivyo.

Kwa sababu aliingiza kichwa na kuupiga mpira kwenye mguu wa beki wa Al Ahly. Mchezaji mwingine angeogopa kuumia, lakini yeye alijitosa kwa ajili ya klabu na mashabiki wake. Haikushangaza alipoonekana na baadhi ya wageni waliokuwa nchini wakiongea naye baada ya mechi kumalizika.

**# Che Malone Fondoh**

Ni mmoja wa mabeki bora kabisa kutoka nje ya nchi waliobahatika kuja nchini Tanzania. Sasa ndiyo mashabiki wanafahamu kwa nini Simba ilikuwa nusura imkose kwani klabu mbalimbali zilikuwa zinamuwania ikiwamo CSKA Sofia ya Bulgaria.

Wengi walibeza kwa Simba kumuacha Joash Onyango na kumsajili Che Malone msimu huu. Lakini sasa kila mmoja amekubali. Katika mechi ya juzi alikuwa mhimili mkubwa kuzima au kupunguza mashambulizi ya pembeni ya Al Ahly.

Tukio kubwa zaidi ambalo mashabiki wengi wanalikumbuka ni kumkimbiza straika aliyekuwa amewaacha mabeki dakika za mwisho akienda kufunga bao la tatu, lakini Mcameroon huyo alikuwa na mbio zaidi, akamkuta akiwa anapiga shuti ili afunge, akapeleka mguu na kuuzuia mpira huo uliotoka nje na kuwa kona, huku benchi zima la Al Ahly likiwa limesimama tayari kwa kushangilia.

**# Henock Inonga**

Ni pacha wa Che Malone, naye pia akiwa mchezaji ambaye alifanya kazi kubwa katika mechi ya ufunguzi wa African Football League.

Pamoja na kuokoa hatari, lakini moja ya kazi aliyokuwa akiifanya ni kuwanyima uhuru mastraika na mawinga wa Al Ahly, wakati mwingine akikimbia na kwenda kujiingiza mbele yao ili wamsukume na kuwa faulo.

Ni mbinu ambazo amekuwa akizitumia mara kadhaa, na katika mechi hiyo alikuwa akizitumia ili kupunguza kasi ya mashabulizi ya pembeni na alifanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Pia aliokoa mpira uliokuwa unatinga wavuni, baada ya kutokea purukushani kwenye lango lao iliyotokana na mpira wa kona.

**# Fabrice Ngoma**

Baada kutoka kwa Mzamiru Yassin, Mkongomani huyo alirudishwa kucheza namba sita, badala ya nane aliyokuwa akiipiga mwanzo.

Nafasi yake ikachukuliwa na Saido Kanoute ambaye alicheza kama 'box-to-box midfielder', akienda mbele na kurudi kumsaidia Ngoma.

Pamoja na kucheza namba sita, lakini bado alikuwa na uwezo wa kuuchukua mpira na kupanda nao mbele, na pasi zake zilikuwa za uhakika na za kiwango cha juu. Kikubwa ni kwamba alikuwa hapotezi pasi, na aina zake ni zile elekezi. Ni mmoja wa wachezaji waliotia fora na kuwavutia wengi kwenye mechi hiyo.

**# Mohamed Hussein 'Tshabalala'**

Licha wa wengi kudai amechoka na umri umeanza kumtupa mkono, lakini alikuwa kwenye kiwango bora kwenye mechi hiyo. Alimfanya winga wa Al Ahly Percy Tau kuwa kwenye wakati mgumu na kutocheza kwa kiwango chake kilichozoeleka.

Inawezekana ilikuwa ni maelekezo ya kocha au yeye mwenyewe kwani Tshabalala hakuonekana kupanda sana kama ilivyo kawaida yake, badala yake alikuwa 'akila sahani moja' na Tau, mmoja wa mawinga bora Afrika raia wa Afrika Kusini.

**JE, WAJUA?**



Arsenal haijapoteza katika mechi za Ligi Kuu England msimu huu, ikiwa imeshinda sita na kutoka sare tatu kwenye mechi tisa ilizocheza hadi sasa.



# Hizi hapa faida za Tanzania kujiunga na IRENA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga amesema kuwa, Tanzania inakusudia kujiunga na mkataba wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati Jadidifu Duniani (IRENA) kutokana na faida zilizopo kwenye mkataba huo.

Miongoni mwa faida hizo ni kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuimarisha upatikanaji wa nishati safi, salama ya uhakika na gharama nafuu pamoja na kupunguza umasikini na kuleta maendeleo endelevu.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini hapa kwenye kikao cha Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kilicholenga kujadili mapendekezo ya Tanzania kujiunga na mkataba huo.

Alisema Tanzania itapata manufaa baada ya kujiunga na mkataba wa IRENA ni pamoja na kunufaika na mikopo mbalimbali ya kufanya utafiti, kuibua na kuendeleza miradi ya nishati jadidifu inayotolewa kwa nchi wanachama na kupata misaada ya kiteknolojia kwa ajili ya uendelezaji wa nishati Jadidifu.

Naye, Katibu Mkuu Wizara hiyo, Mhandisi Felchesmi Mramba alisema kuwa mkataba wa IRENA hauzuii matumizi ya nishati nyingine kama vile gesi na makaa ya mawe, bali unahimiza matumizi ya nishati mbadala na rafiki kwa mazingira.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. David Mathayo alipongeza serikali kwa kuwa na mpango huo wa kujiunga na mkataba wa kimataifa wa nishati jadidifu ili kulinda na kuhifadhi mazingira.

# Serikali yatoa onyo kampuni zinazoficha petroli na dizeli

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imewaonya wafanyabiashara na wamiliki wa vituo vya kuuza mafuta ya dizeli na petroli wanaoficha nishati hiyo, ikisema yeyote atakayebainika atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa utoaji tuzo kwa watoa huduma, waendesha vituo vya Kampuni ya Puma Energy zaidi ya 70.

Judith alisema kumekuа na tabia ya baadhi ya wafanyabiashara wa jumla na rejareja wa nishati ya mafuta ya dizeli na petroli ambao wanaficha kwa makusudi nishati hiyo kwa manufaa yao binafsi.

"Wafanyabiashara wa jumla na wamiliki wa vituo vya mafuta acheni tabia ya kuficha mafuta. Tutachukua hatua kali kwa yeyote atakayebainika," alisema.

Aidha, aliutaka uongozi wa Kampuni ya Puma Energy kuongeza vituo vya kuuza mafuta hususani maeneo ya pembezoni mwa mji hususani vijijini ili kuwafikia Watanzania wengi zaidi.

Pia, aliuomba uongozi wa kampuni hiyo kutoa ufadhiri wa masomo ya mafuta na gesi jwa wanafunzi wa elimu ya juu ili kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan.

"Sote tunajua Rais Samia Suluhu Hassan anafadhiri wanafunzi wa elimu ya juu wanaosoma masomo ya sayansi, hivyo na nyie nawaomba mumuunge mkono Rais Samia katika jitihada hizo, lengo ni kuhakikisha taifa linakuwa na wasomi wengi zaidi," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Puma Energy, Fatma Abdallah, alisema mchakato wa kutoa tuzo na vyeti kwa watoa huduma na waendesha vituo vya puma ulianza mwaka 2020.

Alisema Kampuni ya Puma Energy inahudumia asilimia 20 ya soko la Tanzania katika nishati ya mafuta ya dizeli na petroli.

Alisema kwa sasa wanavituo 74 nchini, ifikapo mwishoni mwa mwaka huu lengo ni kufikisha vituo 80, lengo mama ni kuwa na vituo 120.

Alisema: "Tunataka kila mtanzania anayeishi pembezoni apate huduma ya puma, hii itafikiwa kwa ushirikiano kati ya uongozi na wafanyakazi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Puma Energy, Dk. Selemani Majige, alisema kwa sasa Kampuni ya Puma Energy imeanza kuuza gesi katika Jiji la Dar es Salaam na matarajio ni kuifikisha huduma hiyo mikoa yote.

Alisema pia mikakati ya muda mrefu ya Kampuni ya Puma ni kuanzisha vituo vidogo vitatu maeneo ya vijijini ili kuwawezesha Watanzania kupata huduma ya nishati ya mafuta kwa wepesi.



Rais Samia Suluhu akimkabidhi cheti ya uwakala wa usambazaji wa mkaa mbadala wa rafiki briquettes unaozalishwa na Shirika la Taifa la Madini (STAMICO) Mkurugenzi wa Shirika la Foundation For Disabilities Hope (FDH) Maiko Salali wakati wa uzinduzi wa mitambo ya uchorangaji wa madini kwa wachimabaji wadogo juzi jijini Dodoma. **PICHA: PAUL MABEJA**

# RC aziagiza halmashauri kuvuka malengo ukusanyaji mapato

**Na Augusta Njoji,** KONDOA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule ameagiza halmashauri za mkoa huo kuvuka malengo ya makusanyo katika bajeti iliyotengwa, ili utekelezaji wa miradi ya maendeleo ukamilike kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa.

Akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa Vijijini katika ziara yake ya kukagua na kufuatilia miradi ya maendeleo, Senyamule alisema wanapaswa kutimiza wajibu wao na kufanya kazi kwa weledi na ufanisi katika utekelezaji na usimamizi wa mradi ya maendeleo katika halmashauri hiyo.

"Tunasisitiza ukusanyaji wa mapato kwa kuwa kila sekta imeguswa kwa upande wake, hivyo kila mmoja katika kipande alichopewa ahakikishe anachangia katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwakuwa mchango wa kila mmoja ni muhimu na ni jukumu letu sote katika kuongeza mapato katika maeneo yetu," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Dk.Khamis Mkanachi alisema suala la kuimarisha ukusanyaji wa mapato ni wajibu wa kila mmoja na kusisitiza kuwa bila kuwapo kwa mapato uendeshaji wa halmashauri unakua ni mgumu.

# Tanzania yashiriki maonesho ya kilimo, mazingira Doha

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TANZANIA kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ni miongoni mwa nchi 80 zinazoshiriki maonesho ya Kimataifa ya Bidhaa za Kilimo na Mazingira Jijini Doha, nchini Qatar.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Mazingira Mwandamizi kutoka NEMC, Milton Mponda alisema NEMC inaonesha jinsi kilimo endelevu na uhifadhi wa mazingira ni vitu ambayo haviwezi kutenganishwa kwa kuwa vinategemeana.

Alibainisha kuwa ili kilimo kiwe endelevu na kinachozingatia uhifadhi wa mazingira ni lazima kuzingatia uandaaji wa mashamba ambao unazingatia uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kuzuia mmomonyoko wa udongo kwa kutumia matuta na kupunguza ukataji wa miti na uoto wa asili.

Alifafanua kuwa uvunaji na uhifadhi wa maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji hasa wakati wa kiangazi, matumizi ya mimea kudhibiti wadudu badala ya dawa za viwandani ambazo zina kemikali hatari kwa wanyama, mimea, wadudu na mazingira kwa ujumla.

"Udhibiti wa viuatilifu vilivyoisha muda wake pamoja na vifungashio vyake ili visiingie kwenye vyanzo vya maji na kuleta uharibifu kwenye maji pamoja na mifumo ikolojia, kufungasha bidhaa za kilimo kama vile maua, matunda na mboga kwa kutumia vifungashio vinavyoweza kuoza ambavyo ni rafiki kwa mazingira. Lakini kama kuna ulazima wa kufunga kwenye vifungashio vya plastiki lazima vikidhi kiwango vinavyotakiwa kisheria," alisema.

Aidha, alisema kufanya Tathimini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kwa miradi ya kilimo cha mboga, maua na matunda ili kupata cheti chenye masharti ya usimamizi wa mazingira, usimamizi wa matumizi ya maji katika kilimo cha umwagiliaji kwa kuzingatia urudishwaji wa maji katika mkondo wake, kusakafia mifereji ya maji ili kupunguza upotevu wa maji pamoja kufanya ufuatiliaji wa ubora wa maji kabla ya kuyarudisha katika mkondo wake.

"Jambo lingine la kuzingatia ni kufanya kilimo kinachozingatia uzalishaji wa mazao na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, kilimo kinachozingatia uachaji wa mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji, pia matumizi/uchukuaji wa maji katika mito yanayozingatia watumiaji wengine na viumbe hai kwa ujumla," alisema.

Alisema kufanya 'Green House Farming ili kupunguza ukataji wa miti na uoto, matumizi ya kemikali yaliyokithiri na kudhibiti wadudu vamizi wa mimea na magonjwa.

Ofisa huyo alisema NEMC wametumia maonesho ya Doha Expo 2023 kuelimisha umma uliotembelea Banda la Tanzania jinsi nchi ilivyojidhatiti katika suala la utunzaji wa mazingira katika uwekezaji wa kilimo cha matunda, maua na mboga.

Alisema: "Hii inaweka mazingira wezeshi na rafiki kwa wawekezaji kuja nchini kuwekeza kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Suala la kusajili miradi kwa ajili ya TAM kwa sasa umerahisishwa na unaweza kufanywa ukiwa popote kupitia mfumo maalum wa PMS kwa hiyo wawekezaji wanakaribishwa kusajili miradi yao wakiwa popote".





# Leseni feki zabainika uuzaji mbolea nje ya nchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MFUMO wa ruzuku inayotolewa na serikali kwenye pembejeo za kilimo hasa mbolea, uko hatarini kuhujumiwa na watu wasiokuwa waaminifu kutokana na kubainika kwa matumizi ya leseni feki za uingizaji na uuzaji wa mbolea nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Nchini (TFRA), Dk. Antony Diallo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa alipozungumza na mawakala wa usambazaji wa mbolea ya ruzuku katika mikoa ya Mbeya na Songwe.

Alisema katika ziara zake akiwa kwenye moja ya mipaka alikagua na kubaini uweao wa leseni ya uingizaji wa mbolea nchini ambayo feki lakini inatumika bila kushtukiwa na maofisa wa Forodha.

Alisema leseni hiyo moja ilimfanya ahisi kuwa zipo leseni nyingi za aina zinazoweza kuathiri takwimu za mbolea inayoingizwa nchini pamoja na mbolea ya ruzuku inayotolewa na Serikali kwa wakulima wake.

"Baada ya kubaini kuwa leseni ile feki haikuweza kugundulika kwa maofisa wa Forodha, niliamini kuwa kuna tatizo kwa upande wetu sisi Mamlaka ambalo linahitaji kushughulikiwa haraka iwezekanavyo," alisema Dk. Diallo.

Alisema ili kudhibiti leseni hizo TFRA inatakiwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Maofisa wa Forodha walio mipakani ili waweze kutambua leseni halali na feki.

Alisema hatua nyingine ni kupitia upya mfumo wa utoaji wa leseni hizo kwa lengo la kuongeza udhibiti na kufanya leseni hizo zisighushiwe kirahisi.

Baadhi ya mawakala wa mbolea katika mikoa ya Mbeya na Songwe nao walitumia fursa hiyo kueleza changamoto zinazowakabili kuhusiana na mfumo wa usambazaji wa mbolea ya ruzuku kwa wakulima.

Maisha Silwiwa ambaye ni Wakala wa mbolea wilayani Ileje, alisema kuwa mfumo wa kuuzia wakulima mbolea ya ruzuku sio rafiki kwenye biashara yao kwa kuwa unachukua muda mrefu kumpatia mkulima huduma.

Alisema mkulima anapofika kununua mbolea anahitaji apate huduma haraka ili aende kuendelea na shughuli zake, lakini kutokana na mfumo kuhitaji mchakatio mrefu wa kupitia mpaka kumpatia mkulima huyo huduma, inakuwa kero na kwa mtoa huduma.

Silwimba aliomba serikali kuweka mfumo mwepesi utakaowezesha makala kutoa huduma kirahisi na kwa wepesi lakini hapo hapo kukiwa na udhibiti mzuri wa utoaji wa mbolea hiyo.

"Tunajua lengo la mfumo huu kuwa na mchakato mrefu ni udhibiti, jambo ambalo sio baya, hivyo tunaomba mje na mfumo rahisi na wenye ufanisi bila kuathiri udhibiti," alisema Silwimba.

Naye Gaston Kaduma ambaye ni wakala wa mbolea ya ruzuku wilayani Mbarali mkoani Mbeya, alisema tofauti ndogo ya bei kati ya maeneo ya mijini na vijijini ni chanzo cha mawakala wengi kutopeleka mbolea ya ruzuku mpaka vijijini.

Alisema ikiwa bei ya mjini inafanana au inatofatiana kidogo sana na bei inayopaswa kuuza mbolea vijijini inawafanya mawakala waamue kuuzia mbolea mijini kwa kukwepa gharama za usafiri.

Akizungumzia mikakati ya mkoa wa Mbeya ya kuhakikisha mbolea ya ruzuku inawafikia wakulima hadi vijijini, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema moja ya masharti watakayopewa mawakala ili waweze kusambaza mbolea mkoani Mbeya ni kuhakikisha wanaifikisha mpaka vijijini.



Wafuasi wa CHADEMA wakiwa katika mkutano wa chama hicho wa uzinduzi wa Oparesheni +255 Kanda ya Nyasa, uliofanyika katika viwanja vya Shule ya Sekondari Mwalimu Nyerere, Tunduma Mjini mkoani Songwe juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baadhi viongozi AMCOS watuhumiwa kuhujumu mfumo stakabadhi ghalani

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, imebaini kuwa baadhi ya viongozi wa vyama vya msingi vya wakulima wa kakao (AMCOS) wilayani Kyela wanashiriki kuhujumu mfumo wa stakabadhi ghalani ambao unatumika kwenye zao hilo.

Viongozi hao wanadaiwa kuingiza takwimu zisizokuwa sahihi za magunia ya kakao yanayohifadhiwa kwenye maghala hasa kwa kuandika idadi ya juu kuliko uhalisia na kujipatia fedha isivyo halali.

Hayo yamebainika ikiwa ni wiki moja tangu viongozi hao kwa kushirikiana na watunza maghala kutafuna zaidi ya Sh. milioni 800 za wakulima hali iliyozua malalamiko miongoni mwa wakulima na Mkuu wa mkoa kuagiza viongozi hao kukamatwa na kuswekwa rumande.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Maghela Ndimbo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa anawasilisha ripoti ya uchunguzi kwenye vyama vya msingi vilivyokuwa vinatuhumiwa kushiriki kwenye wizi wa fedha hizo.

Alisema katika uchunguzi walioufanya walibaini baadhi ya viongozi hao walikuwa wanashirikiana na wasimamizi wa maghala ya kuhifadhia kakao ili kuongeza idadi ya magunia kwenye Ankara za mauzo.

Alisema idadi ya magunia iliyokuwa inaongezwa kwenye Ankara za mauzo ilikuwa haiingizwi kwenye kitabu cha walinzi wa maghala hayo (gete pass) ili kupoteza Ushahidi.

"Mfano katika Mnada wa Septemba 4, 2023, Mababu AMCOS iliingiza magunia 65 kwenye kitabu cha ghala la Kikusya lakini kwenye Ankara ya mauzo inaonyesha walishiriki kwa magunia 124, kwahiyo walijiongezea magunia 59 ambayo fedha ziliingia mifukoni mwao," alisema Ndimbo.

Baada ya ripoti hiyo kutolewa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliagiza viongozi wanaoshikiliwa na vyombo vya dola wilayani humo kuendelea kusota mpaka watakaporejesha fedha zote za wakulima ambazo walizitafuna.

Alisema baadhi ya fedha za wakulima ziliingzwa kwenye akaunti za vyama vyao, lakini ndani ya muda mfupi zikaondolewa na viongozi hao wakagawana huku ikionyesha kuwa wakulima walikuwa wameshalipwa fedha zao.

Homera alisema utaratibu ambao umekuwa ukifanywa na viongozi hao ni wa uingizaji wa wakulima hewa kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani hali ambayo inaharibu. Aliliagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kuendelea kuwashikilia viongozi hao mpaka watakaporejesha fedha hizo na wakulima kulipwa.

"Lakini pia viongozi wa AMCOS ambao vyama vyao vimetajwa, wanatakiwa waendelee kuripoti TAKUKURU mpaka wakulima wao watakapokuwa wamelipwa fedha zao, lakini kama uchunguzi utabaini kuwa walishiriki, hatua zaidi zitachukuliwa," alisema Homera.

Aliwataka wakulima kuendelea kuwa wavumilivu wakati jambo hilo likishughulikiwa na atahakikisha wanalipwa fedha zao zote ili waendelee na shughuli zao zingine.

## Waonywa matumizi ya dawa bila ushauri wa daktari

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WALIMU wa shule za sekondari katika Halmashauri ya Mji Njombe, wameshauriwa kuepuka kupata ushauri wa kutumia dawa mtaani badala yake waende kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya ili kuchunguzwa afya zao na kuepuka madhara yatokanayo na matumizi holela ya dawa.

Rai hiyo ilitolewa na mkaguzi wa dawa kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Grace Kapande, wakati akitoa elimu ya matumizi sahihi ya dawa na madhara yatokanayo na matumizi mabaya ya dawa kwa walimu wa shule za sekondari Mabatini, Mbeyela, Yakobi na Uwemba.

"Ninyi wote ni watumishi wa serikali na mna bima za afya niwaombe tumieni hizo bima kuchunguza afya zenu, nenda hospitali usikubali ununue dawa bila kupima ugonjwa wakati bima ya afya unayo na uzuri sasa hivi kwenye hospitali zetu vipimo vingi vinafanyika tupime afya wapendwa," alisema Kapande.

Kapande alisema matumizi mabaya ya dawa ikiwamo kutokumaliza dozi na kutumia dawa bila kupima afya yamesababisha baadhi ya dawa kuonekana hazifanyi kazi kwasababu tayari zimetengeneza usugu wa vimelea vya magonjwa na nyingine kuharibu viungo kwenye mwili wa binadamu.

"Unapopewa dozi ya dawa na mtaalamu hakikisha unamaliza, kumekuwa na tabia mtu anapewa dawa akinywa dozi mbili anapata nafuu anaacha, hiyo ni mbaya ndiyo inasababisha vimelea vinakuwa sugu na ugonjwa kujirudiarudia, kama dozi ni kutwa mara tatu kwa siku tano hakikisha unatumia kila baada ya saa nane bila kupunguza wala kuongeza muda hayo ndiyo matumizi sahihi dawa," alisisitiza Kapande.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mbeyela, Pulkeria Mlwale, alitoa ombi kwa wafamasia wanatoa huduma kwenye vituo vya afya kuendelea kutoa elimu nakusisitiza wagonjwa kutumia dozi kwa usahihi ili kuepuka ugonjwa kujirudia na kuwa sugu.

"Tunawashukuru sana TMDA kwa mafunzo haya, pia msiishie hapa muendelee kutupa elimu ili tujue matumizi sahihi ya dawa kwa sababu ni ukweli kwamba tunatumia dawa bila ya maelekezo ya wataalamu," alisema Mlwale.



# RC aagiza masheha kusimamia vizuri kodi ya majengo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MASHEHA Zanzibar wametakiwa kuwasimamia wamiliki wa majengo katika maeneo yao ili kuhakikisha wanalipa kodi ya majengo, serikali kupata fedha na kufanya shughuli za maendeleo.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Magharibi Unguja, Hamida Mussa Khamis, wakati akifungua kikao kazi kilichowashirikisha masheha na kuwapatia elimu kuhusu kodi ya majengo.

Alisema kodi ya majengo ni sehemu ya ubunifu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuona inapata vyanzo vya ziada vya mapato katika eneo hilo.

Aliwataka masheha kuzitambua nyumba zote zenye sifa kwa ajili ya kutozwa kodi ya majengo ikiwemo za biashara na nyumba za ghorofa.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar, Yussuf Juma Mwenda, alisema serikali imekuja na marekebisho ya sheria ya kuanzisha kodi ya majengo hatua ambayo itasaidia katika ukusanyaji wa mapato.

Hivyo, aliwataka wananchi kuondoa wasiwasi na kwamba kodi ya majengo itakusanywa kwa wamiliki wa nyumba za ghorofa pamoja na zile zinazofanya biashara kuanzia Sh.50,00 na haitajumuisha nyumba za watu wa kawaida.

Baadhi ya masheha walifurahishwa na kupewa elimu juu ya kodi ya majengo ambapo awali ulikuwepo wasiwasi mkubwa kwa wananchi wa kawaida kwamba wanakwenda kutozwa kodi ya nyumba.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano wa huduma za mlipa kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZMA), Shaaban Yahya Ramadhan, alisema kodi hiyo sio mpya kwa sababu sheria yake ilipitishwa tangu mwaka 2008 lakini haikuweza kufanya kazi kwa sababu mbali mbali.

Alisema sheria hiyo imeanza kutumika rasmi katika mwaka 2023 katika bajeti ya serikali ambayo lengo lake ni kuongeza mapato ya serikali katika kukuza uchumi.

Aliyataja majengo yatakayoidhinishwa kwa ajili ya kulipa kodi ni hoteli za nyota tano Sh.500,000, hoteli za nyota nne Sh.400,000 pamoja na majengo ya biashara yenye ghorofa Sh.50,000, huku nyumba za makazi ni Sh.10,000.

**Aliwataka masheha kuzitambua nyumba zote zenye sifa kwa ajili ya kutozwa kodi ya majengo ikiwemo za biashara na nyumba za ghorofa.**

# Waandishi wa vitabu watakiwa kuhifadhi utamaduni Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Mohammed Said amewataka waandishi wa vitabu vya fasihi kuhifadhi utamaduni wa mzanzibari ili kurithiwa na vizazi vijavyo.

Aliyasema hayo katika ufunguzi wa tamasha la kwanza la vitabu vya Zanzibar ulioambatana na uzinduzi wa Kitabu cha Peponi kilichoandikwa na Professa Gurnah mshindi wa Tunzo ya Nobel.

Alisema ni muhumu kwa waandishi kuendeleza utamaduni unaohamasisha umoja na upendo, badala ya kuchochea vurugu jambo ambalo ni kinyume na malengo ya uandishi wa vitabu hivyo.

Alisema Zanzibar ni kitovu cha fasihi bora na imetoa waandishi mashuhuri ambao wamejipatia umaarufu duniani na hivyo kusaidia kuitangaza Zanzibar kitaifa na kimataifa.

Alisema ushindi wa kitabu cha fasihi simulizi cha Peponi kimeamsha hari kwa watunzi vijana kufanya kazi za utunzi kwa kufikia malengo makubwa. Alisema Zanzibar imebahatika kuwa na utajiri wa magwiji wa vitabu vya fasihi simulizi ambao kwa kiasi kikubwa unatokana na asili ya kuwa na chemchemu katika matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu.

"Niipongeze sana Jumuiya ya Vitabu Zanzibar (ZBF) kwa maandalizi mazuri ya Tamasha hili na Serikali italiendeleza na kulikuza kwasababu linaongeza idadi ya matamasha yanayoitangaza Zanzibar kimataifa" alisema.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum aliwataka waandishi wa vitabu kuitumia mitandao ya kijamii katika kutuma vitabu vyao ili kuwafikia wasomaji wengi.

Mkurugenzi wa Jumuiya ya Vitabu, Ally Baharoon, alisema tamasha hilo ni muhimu na litachangia kuwakutanisha waandishi wa kitaifa na kimataifa ili kujengeana uzoefu katika kazi zao za utunzi wa vitabu.

Mtunzi wa Kitabu cha "Peponi" ambacho kimepata tuzo ya kimataifa ya Nobel ya mwaka 2021, Professa Abdurazak Gurnah, aliwataka watunzi wa riwaya wasikate tamaa kwa sababu utunzi wa kitabu huchukua muda mrefu.

Akitolea mfano alisema yeye ilimchukuwa zaidi ya miaka 40 ya kutunga vitabu na baadaye kuibuka na heshima ya juu ya kimataifa ya fasihi.

Alisema kutunga vitabu si kazi rahisi inayohitaji uvumilivu wa hali ya juu pamoja na kutumia muda mwingi katika kujisomea.

"Nilianza kuandika vitabu nikiwa na umri wa miaka 18, baada ya kuondoka Zanzibar kuelekea nchini Uingereza katika safari ambayo ni ngumu katika maisha yangu" alisema.

Aidha, alisema ameandika vitabu mbalimbali lakini kitabu cha Peponi ndiyo kikamuibua na ushindi wa Tuzo ya Nobel ya Fasihi na kutambulikana duniani kote.

Mchapishaji maarufu wa Kampuni ya Mkuki na Nyota ambayo imekitafsiri Kitabu cha "Paradise" kwa lugha ya Kiswahili, Walter Bgoya alisema wamechukuwa jukumu la kukitafsiri kitabu hicho ambacho kimebeba utajiri mkubwa wa kazi za fasihi simulizi duniani.



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Mohammed Said akikata utepe kuashiria uzinduzi wa kitabu cha 'Peponi' kilichoandikwa na Prof.Abdulrazak Gurnah na kutafsiriwa na Dk Ida Hadjivayanis katika tamasha la kwanza la vitabu lililofanyika Ukumbi wa Shekhe Idris Abdul Wakil, Kikwajuni Mjini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yabuni mbinu mpya kuvutia watalii misimu yote

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Vijana, Michezo na Utamaduni, Tabia Maulid Mwita alisema serikali imeweka mikakati ya kuhakikisha haitegemei wageni katika msimu wa utalii, hivyo imeibua mbinu mbadala ya kuhakikisha watalii wanafika Zanzibar kipindi chote.

Alisema miongoni mwa mbinu hizo ni kufanyika kwa matamasha yakiwemo ya michezo ambayo yataongoza ujio wa watalii na kuongeza pato la taifa.

Aliyasema hayo Zanzibar wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ujio wa tamasha la michezo la kimataifa ambalo linatarajia kufanyika Februari mwakani.

Alisema tamasha hilo litasaidia kuinua sekta ya utalii na vijana kuonesha uwezo wao na vipaji katika michezo hatua ambayo itaongeza ajira.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga kuimarisha sekta ya utalii na kuufanya mwaka mzima kutembelewa na wageni ikiwemo kuandaa matamasha ya kimataifa ya utalii ambayo yatatangaza vyanzo na vivutio vyake ikiwemo majengo ya kale yaliyobeba historia kwa watawala mbalimbali" alisema.

Alisema kuwepo kwa tamasha hilo ni fursa nyingine kwa wananchi wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kuonesha vipaji katika michezo ambayo imekuwa ikipata umaarufu duniani ikiwemo riadha pamoja na mchezo wa kriketi.

Aidha, alisema baadhi ya matamasha mengine ambayo yanatarajiwa kutangaza sekta ya utalii katika maeneo mbalimbali ni tamasha la vitabu vya fasihi simulizi ambalo litasaidia kutangaza lugha ya Kiswahili.

Mkurugenzi wa Masoko wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Rahma Mohamed Sanya, alisema kufanyika matamasha ya michezo ni sehemu ya ubunifu katika kukuza michezo pamoja na kuwavutia watalii kufika Zanzibar.

Alisema sekta ya utalii inazidi kupata mafanikio makubwa ambapo asilimia 30 ya mapato ya serikali yanayokusanywa yanatokana na ukuaji wa sekta hiyo ikiwemo uwekezaji katika hoteli zenye hadhi ya nyota tano.

# Hichilema afurahishwa uwekezaji wa Taifa Gas

**Na Mwandishi Wetu, LUSAKA**

Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, amefurahishwa na uamuzi wa kampuni ya Tanzania ya Taifa Gas, kuingia ubia na kampuni ya Zambia, Delta Marimba na kuwekeza katika uzalishaji umeme nchini humo.

Kampuni inayomilikiwa na mfanyabiashara maarufu nchini, Rostam Aziz, ya Taifa Gas, imeungana na kampuni ya Zambia, Delta Marimba, na kuunda kampuni ya Taifa Marimba ambayo imetenga kiasi cha dola milioni 100 za Marekani katika uwekezaji huo wa awali.

Akizungumza Ikulu ya Zambia mwisho mwa wiki baada ya Aziz na ujumbe wake kumtembelea, Rais Hichelema alisema kuwa hatua ya kampuni za Afrika kuungana na kuwekezeza katika nchi zao ni ya kupigiwa mfano.

"Hii ndio njia tya haraka itakayoliwezesha bara la Afrika kuondokana na kuwa chanzo cha malighafi kwa ajili ya viwanda vya nchi nyingine," alisema Rais Hichelema.

Katika uwekezaji huo wa awali kampuni ya Taifa Marimba imepanga kugeuza mitambo ya kuzalisha umeme inayotumia dizeli na kuiwezesha kutumia gesi.

Licha ya unafuu wake wa bei, lakini pia gesi inapatikana kirahisi na ni moja ya nishati ambazo hazichangii uharibifu wa mazingira.

Rais Hichelema na Aziz walisisitiza kukuza biashara na uwekezaji baina ya nchi za Afrika kuwa ndio njia pekee ya nchi hizo kusaidiana na kuimarisha uchumi wao kwa haraka badala ya kuwategemea watu wengine kutoka nje ya bara hilo.

Rais Hichelema alibainisha kuwa serikali yake inalenga uzalishaji wa umeme na usambazaji wake unaongezeka nchini humu na uwekezaji huu wa Taifa Marimba ni muhimu sana kufanikisha hilo.

Alisema inafurahisha kuona kampuni kutoka nchi mbili zinaungana ili kutafuta suluhisho la matatizo yanayowakabili wananchi wa Zambia na iwapo kampuni nyingine zitaiga mfano huo basi Waafrika wenyewe wanaweza kuyatatua matatizo mengi yanayowakabili.

Kwa mujibu wa Aziz, uwekezaji huo wa awali unalenga kuzalisha umeme kwa ajili ya sekta ya madini, lakini hapo baadaye utapanuliwa kwenye sekta nyingine pia.

"Na kwa mujibu wa mipango yetu uwekezaji utahusisha pia uzalishaji wa umeme kwa kutumia nguvu za jua na pia upepo. Pia baadaye tutawekeza kwenye maeneo mengine nje ya uzalishaji umeme," alisema Aziz.

Alisema Taifa Marimba imeamua kufanya uwekezaji huo kama njia ya kuimarisha uhusiano wa karibu, wa kidugu na wa kihistoria kati ya Zambia na Tanzania huku wakiamini kuwa kuunganisha nguvu kwa kampuni za Afrika kutaziwezesha kufanya mambo mengi makubwa.

Rais Hicheklema alizihimiza kampuni za Zambia kutafuta wabia nje na ndani ya nchi kwa ajili ya kufanya miradi mikubwa ya kiuchumi na kijamii.

Aziz alimhakikishia Rais Hichelema kuwa Taifa Gas itaedelea kuwekeza nchini humo kwani kuna fursa nyingi za uwekezaji.

"Na pia tutakuwa mabalozi wazuri wa kuzihimiza kampuni nyingine kutoka katika ukanda huu kuungana na kuja kuwekeza Zambia," alisisitiza.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Delta Marimba, Padmore Muleya, alisema upembuzi wa awali wa kiwanda cha kuzalisha umeme kutokana na gesi unaendelea vema na wanafurahi kuwa serikali inawaunga mkono.

"Mipango yetu ni kuhakikisha tunaanza uzalishaji wa umeme ndani ya miezi 24 ijayo," alisema.

Zambia inakuwa ni nchi ya pili katika ukanda huu kwa kampuni ya Taifa Gas kuwekeza baada ya kuingia nchini kenya ambako kampuni hiyo inajenga mtambo wa kuchakata gesi ya kupikia jijini Mombasa.



Balozi wa China nchini Tanzania, Chen Ming Jiang aliesimama akitoa nasaha zake kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam muda mfupi kabla ya kwenda nchini China kwa mafunzo ya miaka miwili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mwigulu aiagiza PPRA kuunganisha mfumo serikalini

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ameiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kuunganisha haraka mfumo wa ununuzi serikalini wa NeST na GIMIS ili isomane.

Amesema mifumo hiyo itawezesha wizara, mashirika ya umma, wakala, ofisi za mikoa na halmashauri za wilaya nchini kupata huduma za Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA).

Dk. Mwigulu, alisema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa kwenye hafla ya uzinduzi wa mifumo ya ununuzi serikali ya GIMIS na uzinduzi wa majengo mapya ya GPSA.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amekuwa akisisitiza mifumo ya serikali kusomana, hivyo ninaelekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kuhakikisha wanaunganisha mfumo wa NeST na GIMIS haraka iwezekanavyo kwa kuwa mfumo huu unatumiwa na wizara, mashirika ya umma, wakala, ofisi za mikoa na halmashauri za wilaya nchini katika kupata huduma za GPSA," alisema.

Aliagiza mifumo mingine ihakikishe inaunganishwa na GIMIS ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya wakala.

Aidha, alisema taasisi za nunuzi zinapaswa kutumia huduma za GPSA, kwa kuwa sheria ya ununuzi na kanuni zake inawataka kupata huduma na vifaa mtambuka kupita GPSA.

"Ni imani yangu kuwa katika mpango mkakati wa wakala kwa mwaka 2022/2023 hadi 2027/2028 mtatekeleza kwa kiwango kikubwa zaidi na kupiga hatua kubwa katika utoaji wa huduma kwa serikali na taasisi zake," alisema Dk. Nchemba.

"Ni imani yangu mtaendelea kuchangia katika mfuko mkuu wa serikali kwa mujibu wa sheria ili serikali iweze kutekeleza mipango mbalimbali iliyojiwekea," alisema.

Pia, aliwapongeza wadau wote walioshiriki katika ujenzi wa mfumo ikiwamo Mamlaka ya Serikali Mtandao akiwa ndio mjenzi wa mfumo huo, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi.

"Naomba pia, niwashukuru wadau walioshiriki katika ujenzi wa majengo mapya ni kianza na Shirika la Nyumba la Taifa akiwa ndio mbunifu na mjenzi na SUMAJKT akiwa ndio mshauri mwelekezi"alisema

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora, George Simbachawene, alisema mifumo hiyo itaisaidia serikali kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma.

"Mifumo hii imesanifiwa na imeonyesha mafanikio makubwa na hadi sasa takribani taasisi zaidi ya 7070 zimeshaunganishwa na mifumo hii ya ununuzi serikali," alisema Simbachawene.

## Shule zatakiwa kuwekeza kwenye TEHAMA

**Na Joseph Mwendapole**

SHULE nchini zimeshauriwa kuwekeza kwenye Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na maabara za kisasa ili kulisaidia taifa kupata wataalamu wengi kufanyakazi kwenye sekta ya uhandisi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Kampasi ya Mwanza, Dk Robert Mashenene, wakati akizungumza kwenye mahafali ya 22 ya Shule ya Sekondari St Mary's.

"Dunia inakwenda kasi sana kwahiyo tunavyozidi kuingia kwenye dijitali watahitajika wataalamu wengi sana wa TEHAMA wekezeni katika maabara zenye zana zote za kisasa tuongeze idadi ya wahandisi watakaotumika kwenye miradi mikubwa ya ujenzi," alisema.

"Lazima mjitofautishe na wengine kwa kuwa na maabara za kisasa ambazo zitasaidia kupata wanasayansi wazuri ambao wanahitajika kwenye dunia ya kidijitali," alisema.

Katika hatua nyingine, alisema (CBE), itaiunganisha shule hiyo na Maktaba Kuu ya Taifa ili iwe inapata vitabu mbalimbali.

Alisema vitabu ni nyenzo muhimu kwa wanafunzi hivyo atafanya jitihada ili ndani ya muda mfupi shule hiyo iwe imeunganishwa na maktaba kuu ya taifa na kuanza kunufaika na vitabu vinavyopatikana ndani ya maktaba zake.

Aliwataka walimu na watumishi wote wa shule hiyo washikamane kwani mafanikio waliyopata ni matokeo ya mshikamano na kufanyakazi kama timu moja.

Aliwataka wahitimu wasidhani kuwa kumaliza kidato cha nne ndiyo mwisho wa masomo na badala yake waone kwamba safari ndiyo kwanza imeanza na waendelee kufanya vizuri kwenye masomo.

"Kuna watakaoenda kidato cha tano na wengine vyuoni lakini cha msingi ni nidhamu kokote mtakapokuwa kwasababu nidhamu ni jambo la msingi maishani, nimefarijika sana kuona kuna walimu wanaofundisha maadili na dini," alisema.

Aliwataka wazazi kuwahimiza watoto wao kwenda kwenye nyumba za ibada ambako watajengwa kuishi maisha yenye maadili.

Alisema wazazi wanawajibu wa kufuatilia nyendo za watoto kuanzia mavazi na makundi wanayokuwa nayo kwani wanaweza kupoteza mwelekeo wasipodhibitiwa kuwa na mwenendo mwema.

Aliwataka pia watumie simu kufanya mambo ya msingi badala ya kuitumia kwa mambo machafu na yasiyofaa ambayo yamekuwa chanzo cha mmomonyoko wa maadili.

Pia, kuweka utaratibu wa kuwatafuta wahitimu wa miaka ya nyuma na kuwaalika kwenye mahafali ya shule hiyo kama njia ya kuwahamasisha wanafunzi hao kusoma.

# Utekelezaji haki za watoto nchini waundiwa mkakati

**Na Mwandishi Wetu**

KUCHANGIA utekelezaji wa haki za watoto, vijana na makundi mengine yenye hali duni, asasi ya NMB Foundation na shirika la Save the Children International zimeunganisha nguvu kusaidia kuboresha maisha nchini kwa kuingia makubaliano ya kushirikiana.

Mashirika hayo mawili yalitia saini mkataba wa ushirikiano kwenye shughuli za ustawi wa jamii mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam katika makao makuu ya Benki ya NMB.

Wakati NMB Foundation ni asasi ya kiraia ya NMB, Save the Children ni shirika la kimataifa linaloongoza katika kusimamia haki za watoto. Pia linajihusisha na masuala ya vijana na watu wengine wenye changamoto za kimaisha.

Kabla ya utiaji saini makubaliano hayo, Meneja Mkuu wa NMB Foundation, Nelson Karumuna, alisema ushirikiano huo unalenga kuendeleza mshikamano na uwekezaji katika ustawi na maendeleo ya jamii.

"Tunaingia makubaliano ya kihistoria kati yetu NMB Foundation na wenzetu wa Save the Children yenye lengo la kuimarisha utekelezaji wa haki za watoto, vijana na wanawake nchini.

"Ushirikiano huu ni muhimu kwa kuleta mabadiliko chanya na ya kudumu katika maisha ya Watanzania. Kwa kutumia utaalamu wetu, rasilimali zetu na ubunifu wetu, tunaweza kuziwezesha jamii kwa zana na maarifa yanayohitajika ili kuweza kujitegemea," alisema.

Huku akisisitiza kuwa NMB Foundation itatumia zaidi uzoefu wa miaka mingi wa Save the Children katika shughuli za kibinadamu, Karumuna alisema ushirikiano huo utazingatia zaidi maeneo matano ambayo ni elimu, afya, mabadiliko ya tabianchi na ulinzi wa mtoto.

Shirika hilo lisilo la kiserikali ambalo lengo lake kuu ni kuhakikisha watoto siyo tu wanaishi, bali pia wanastawi, limo nchini tangu mwaka 1986.

"Ushirikiano huu na kuunganisha nguvu kati yetu, ni hatua muhimu kuelekea kutimiza lengo moja ambalo ni kuleta matokeo chanya katika maisha ya watoto, vijana na makundi mengine ya watu wenye hali duni katika jamii zetu," mkurugenzi wake nchini, Anjela Kauleni alisema.

Aliongeza kuwa uamuzi ya NMB Foundation kushirikiana na Save the Children ni uthibitisho wa dhamira yake ya kuchangia kuboresha maisha ya jamii zinazoishi katika mazingira magumu.

Anjela alisema moja ya faida kubwa za ushirikiano huo ni pamoja na taasisi hizo kuimarisha programu za shughuli zao na kupanua wigo wa manufaa yatakayopatikana.

Utiaji wa saini makubaliano hayo ulishuhudiwa na mkurugenzi wa eneo la Afrika Mashariki na Kusini wa Save the Children, Ian Vale, aliyesema ushirikiano huo ni fursa nzuri kwao kufanya kazi na sekta binafsi kusaidia kuboresha maisha.



Wapalestina wakiangalia sehemu ya madhara ya mashambulizi ya Israel kwenye kiunga cha Rafah kusini mwa Gaza, jana. **PICHA: MTANDAO.**

## Museveni ataka wananchi wahusishwe vita dhidi ya ADF

**KAMPALA, Uganda**

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni ameliagiza Jeshi la nchini mwake kuwahusisha wananchi katika juhudi zao za kuwasaka wanamgambo wa kundi la kigaidi la 'Allied Democratic Force' (ADF).

Wiki iliyopita wanamgambo hao walifanya mashambulizi katika mbuga ya kitaifa nchini humo ya Malkia Elizabeth ambako raia wawili wa kigeni na mmoja wa Uganda waliuawa.

Rais Museveni alitoa maelekezo hayo jana, huku akieleza kwamba shughuli za kuwasaka watu hao waliotekeleza shambulizi hilo zinaendelea akiongeza kuwa msako pia unawalenga waliochoma moto lori moja mjini Kasese.

Kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa X - zamani ikiitwa Twitter, Rais Museveni anasisitiza kwamba, 'UPDF inapaswa kuihusisha idara ya polisi na wananchi kusaka hayo makundi yanayodaiwa kutokea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

"Watu hawa siyo tatizo la jeshi pekee yake, ni jukumu la vitengo mbalimbali vya usalama kama polisi, idara ya ujasusi na kila mmoja wetu kuhakikisha vita dhidi ya ugaidi vinafaulu," alisema Rais Museveni.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, jeshi la UPDF lilitekeleza shambulizi katika kambi ya kundi la kigaidi la ADF katika eneo la magharibi mwa DRC ambako jeshi la Uganda linasema kambi kuu ya ADF ililengwa na kuharibiwa.

**BBC**

***Zimekusanywa na Maulid Mmbaga**

# WHO yasisitiza mambo sita kwa Israel

**TEL-AVIV, Israel**

SHIRIKA la Afya Duniani ((WHO) limesisitiza Israel mambo sita ikiwamo kusitishwa mapigano ya kibinadamu na upatikanaji haraka wa misaada bila vikwazo kote Gaza ili kuruhusu wahisani kufikia raia wanaohitaji msaada wa haraka kuokoa maisha na kuzuia mateso zaidi ya kibinadamu.

WHO ilitoa wito huo kupitia taarifa yake iliyoitoa jana, ikiwa ni siku moja baada ya misaada kuanza kuingia rasmi Gaza, huku ukisisitiza kwamba mitiririko ya misaada ya kibinadamu lazima iwe kwa kiwango kikubwa na endelevu na kuruhusu watu wa Gaza wote kuhifadhi utu wao.

Pia ilitoa wito kwa upatikanaji salama na endelevu wa maji, chakula, afya na mafuta yaliyotajwa kuwa ni muhimu katika kuwezesha baadhi ya huduma za kibinadamu katika ukanda huo wa Gaza.

"Tunatoa wito wa ulinzi wa raia wote na miundombinu ya kiraia katika ukanda wa Gaza, ikiwa ni pamoja na vituo vya afya. Ulinzi wa wafanyakazi wa kibinadamu ambao wanahatarisha maisha yao katika kuwahudumia wengine.

"Na tunatoa wito kwa pande zote kuheshimiwa kwa sheria ya kimataifa ya kibinadamu. Gaza ilikuwa na hali ya kukata tamaa kabla ya uhasama wa hivi karibuni. Sasa ni janga. Ulimwengu lazima ufanye zaidi," WHO iilieleza katika taarifa yake hiyo.

WHO ilieleza kuwa zaidi ya watu milioni 1.6 huko Gaza wanahitaji misaada ya kibinadamu. Huku watoto, wanawake wajawazito na wazee wakibaki kuwa hatarini zaidi, kwa kuwa karibu nusu ya wakazi wote wa Gaza ni watoto.

Ilieleza kuwa miundombinu mingi ya kiraia huko Gaza imeharibiwa kutokana mzozo ulioibuka kati ya Hamas na Israel ikijumuisha makazi, vituo vya afya, maji, vyoo na mifumo ya umeme, huku vifo vikiongezeka kutokana na milipuko ya magonjwa, na ukosefu wa afya njema.

"Hospitali zimezidiwa na majeruhi. Raia wanakabiliwa na changamoto zinazoongezeka katika kupata mahitaji muhimu ya chakula. Vituo vya afya havina mafuta tena na vinatumia kiasi kidogo walichopata ndani ya nchi. Na kinatarajiwa kuisha katika siku inayofuata au zaidi.

"Uwezo wa uzalishaji wa maji uko katika asilimia tano ya viwango vya kawaida. Vifaa vya kibinadamu vilivyowekwa tayari vimepungua. Watu wanaoishi katika mazingira magumu wako katika hatari kubwa zaidi na watoto wanakufa kwa kasi ya kutisha na kunyimwa haki yao ya ulinzi, chakula, maji na huduma za afya," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Hata hivyo, ilibainisha kuwa takriban theluthi moja ya wakazi wa Palestina walikuwa na uhaba wa chakula kabla ya mzozo huu huko Gaza. Na kwamba kwa sasa akiba katika maduka zinakaribia kuisha na maduka ya kuoka mikate yanafungwa, huku maelfu ya watu wameyahama makazi yao na hawawezi kupika au kununua chakula kwa usalama.

**SYRIA YASHAMBULIWA**

Licha ya wito wa kusitisha mapambano, kwa mujibu wa DW, ndege za kivita za Israel zimeyashambulia maeneo kadhaa mjini Gaza pamoja na viwanja viwili vya ndege nchini Syria na pia msikiti mmoja katika eneo la Ukingo wa Magharibi unaodaiwa kutumiwa na wanamgambo wa Hamas.

Ilibainishwa kuwa mashambulizi hayo ya usiku wa kuamkia jana yalifanyika wakati malori yaliyosheheni misaada ya kibinadamu yakianza kuingia katika eneo lililozingirwa la Gaza.

Msemaji wa Jeshi la Israel alisema nchi hiyo inaongeza mashambulizi yake ya anga na kuna matarajio pia ya vikosi vya ardhini kuanzisha mashambulizi katika eneo hilo.

Vita hivyo vilivyoingia siku yake ya 16 vinatajwa kuwa vita vikali zaidi kwa pande zote mbili, kati ya vita vitano vilivyowahi kushuhudiwa katika ukanda huo baina ya Israel na kundi la Hamas.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya ya Gaza, watu 4,385, wameuawa hadi sasa huku wengine 13,561 wakijeruhiwa.

Vilevile, Israel ilisema inaamini watu 212 wamechukuliwa mateka na wanamgambo wa Hamas wakati walipofanya mashambulizi yake dhidi ya taifa hilo Oktoba Saba na kuwaua zaidi ya watu 1,400.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**MWANZA**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 12/2023**
**WILFRED NATHANIEL LUHAMA..........MDAI**
**DHIDI YA**

- **LAMECK INNOCENT KAYEBA**
- **NGHUSELA TANZANIA LIMITED.......WADAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: 1) LAMECK INNOCENT KAYEBA**
**2) NGHUSELA TANZANIA LIMITED**

SHAURI LIMEPANGWA KUSIKILIZWA MNAMO TAREHE 07/11/2023 SAA 3:00 ASUBUHI MBELE YA MH.B.M. LEMA-SRM.
MNATAKIWA KUWEPO, AU KUWAKILISHWA KISHERIA PAMOJA NA KULETA UTETEZI WENU DHIDI YA SHAURI HILI.
ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWENU TAREHE HIYO, SHAURI LITAANZA KUSIKLIZWA BILA NYINYI KUTAARIFIWA TENA NA MAAMUZI KUTOLEWA.
IMETOLEWA KWA MKONO WANGU NA MHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 18/10/2023.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI
MWANZA

HABARI MICHEZO

# RICARDO AGEUZIA 'MITUTU' YA SINGIDA FG KWA YANGA

Na Saada Akida

BAADA ya kufanikiwa kuvuna alama tatu ugenini dhidi ya Namungo FC, Kocha Mkuu wa Singida Fountain Gate FC, Ricardo Ferreira, ameweka wazi kuwa anahitaji alama tatu katika mchezo wao ujao dhidi ya Yanga.

Singida Fountain Gate FC juzi walifanikiwa kupata alama tatu kwa ushindi wa mabao 3-2 mbele ya wenyeji wao, Namungo FC katika Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Ferreira alisema mechi dhidi ya Namungo FC ilikuwa ya ushindani mkubwa, wachezaji walipambana na kufanikiwa kuvuna pointi tatu ugenini .

Alisema matokeo ya mechi hiyo hayatawafanya kujiona wako bora bali watatumia changamoto za mechi hiyo kujipanga kwa ajili ya mechi yao yao ijayo dhidi ya Yanga.

"Tumepata alama tatu ugenini, vijana wamepambana, tunarudia Dar es Salaam kujiandaa dhidi ya Yanga kuhakikisha tunafikia malengo yetu ya kutaka kutafuta pointi katika michezo hii mitatu ya mwanzo tangu nilipokabidhiwa timu wiki iliyopita.

"Huu ni ushindi wa kwanza kwangu na mwisho wa mechi hii ni mwanzo wa maandalizi ya mechi yetu ijayo ambayo tunaenda kucheza na Yanga wakiwa nyumbani," alisema kocha huyo aliyedai kuwa anaendelea kuwafuatilia wapinzania wake hao.

Katika mchezo huo, utakaopigwa Oktoba, 26, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Singida Fountain Gate FC itakuwa ugenini.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari St Mary's Mbezi Beach wakionesha umahiri wao kwenye mitindo ya mavazi wakati wa mahafali ya 22 ya kidato cha nne ya shule hiyo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Chanongo aipaisha Pamba, Championship

Na Adam Fungamwango

WINGA wa zamani wa Klabu ya Simba, Haruna Chanongo, juzi aliiwezesha Pamba FC kupata ushindi wa mabao 2-1 katika mechi ya raundi ya saba ya Ligi ya Championship dhidi ya Transit Camp kutoka Dar es Salaam.

Katika mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza, Chanongo ambaye alizichezea klabu mbalimbali za Ligi Kuu ikiwamo Mtibwa Sugar, alifunga bao la pili dakika ya 78 lililoipa pointi tatu Pamba ambayo kwa misimu mitatu sasa inasaka nafasi ya kupanda Ligi Kuu bila mafanikio.

Kabla ya kufunga bao hilo, Chanongo alikosa mkwaju wa penalti wakati timu yake ikiwa sare ya bao 1-1, hadi pale aliporekebisha makosa yake.

Haukuwa ushindi mwepesi kwa Pamba, kwani ilijikuta ikipachikwa bao dakika ya 30 lililowekwa wavuni na straika wa zamani wa Yanga, Idd Mbaga.

Dakika moja tu baada ya Transit Camp kupata bao, Pamba ilisawazisha kupitia kwa Ismail Ali kwa shuti kali la mguu wa kushoto.

Kwa ushindi huo, Pamba inakwea hadi nafasi ya tatu ikiwa na pointi 14 kwa mechi saba ilizocheza, Transit Camp ikiwa nafasi ya 14 kwa na pointi zake nne.

Timu ya KenGold imekwea hadi kileleni kwa msimamo wa ligi hiyo baada ya kuitwanga Cosmopoitan mabao 2-0, mechi ikichezwa Uwanja wa Sokoine Mbeya.

Kwa sasa inaongoza ligi ikiwa na pointi 16 na mabao 13, huku nafasi ya pili ikishikiliwa na Mbeya Kwanza ambao nayo juzi ilipata ushindi ugenini, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha wa mabao 2-1 dhidi ya Mbuni FC.

Mbeya kwanza ina pointi 16 kama KenGold, lakini ina mabao 11 tu ya kufunga. Nayo timu ya Pan African, ikiwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, ililazimishwa suluhu dhidi ya Mbeya City.

# St Mary's yaanza kusaka vipaji vya michezo

Na Joseph Mwendapole

SHULE ya Sekondari St. Marys Mbezi Beach imesema imejenga viwanja vya michezo mbalimbali shuleni hapo kama moja ya njia ya kuhamasisha wanafunzi kupenda michezo na kuibua vipaji vya wanafunzi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa shule hiyo, Ntipoo Reca, wakati wa mahafali ya 22 ya shule hiyo yaliyofanyika shuleni hapo Mbezi Beach.

Reca alisema shule hiyo imepanga muda maalum kwa wanafunzi kushiriki michezo mbalimbali kama mpira wa miguu, mpira wa mikono, sarakasi na skauti ili wanafunzi kuwa wakakamavu.

"Shule pamoja na kufanya vizuri kitaaluma, imeona umuhimu wa kujenga viwanja vya Volleyball, mpira wa miguu, mpira wa kikapu sisi masuala ya michezo hatuyachukulii poa kwa sababu tunafahamu kwamba michezo ni uchumi kwani wapo watu ambao wanaingiza mabilioni kupitia vipaji vyao kwenye michezo mbalimbali," alisema.

"Na tunaushukuru sana uongozi wa shule kwa kutuunga mkono kwenye michezo na kwenye viwanja hivi wameweka taa kubwa kama zinazotumika kwenye viwanja vikubwa vya michezo hali ambayo inasaidia wanafunzi kufanya mazoezi hata nyakati za usiku," alisema.

Mmoja wa wazazi, Anita John, alielezea kufurahishwa na vipaji vilivyooneshwa na wanafunzi hao na kuitaka shule hiyo kuendelea kuibua vipaji vya wanafunzi kwani wako watu wengi wamefanikiwa kupitia sekta hiyo.

"Tumefurahi kuona vipaji vya wanafunzi hawa kwenye michezo mbalimbali na duniani hapa ziko njia nyingi za kufikia mafanikio kwa hiyo kuna mwanafunzi anaweza asiwe mzuri sana darasani lakini akawa na kipaji kwenye kuimba, mpira wa miguu, kikapu na vikampa mafanikio makubwa sana kwa hiyo ningependa shule zingine nazo ziwe na program za kuibua vipaji," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LEWEN OFA NONO SAUDIA
MSHAMBULIAJI wa Everton na England, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 26, anatazamiwa kupewa ofa nono na Klabu ya Saudi Arabia Al-Ettifaq, inayonolewa na Steven Gerrard. **(Sun)**

### MOLINA MKATABA MREFU
KLABU ya Atletico Madrid inataka kumpata mlinzi wa Argentina mwenye umri wa miaka 25, Nahuel Molina, mkataba mpya wa muda mrefu baada ya kuhusishwa na klabu nyingi kubwa. **(Fichajes)**

### PHILLIPS KUONDOKA CITY
KLABU ya Manchester City itamruhusu kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 27, kuondoka katika klabu hiyo katika dirisha la uhamisho la Januari. **(Star)**

### PAGUETA AWINDWA ETIHAD
MANCHESTER City inaendelea kuwa na nia ya kutaka kumnunua, Lucas Paqueta wa West Ham. **(Teamtalk)**

### POTTER AITAKA UNITED
NAPOLI inataka kuzungumza na kocha wa zamani wa Brighton na Chelsea, Graham Potter, kuhusu kuwa kocha wao mpya, lakini Potter anaweza kuwania kuwa kocha wa Manchester United ikiwa Erik ten Hag atafukuzwa. **(Sun)**

### CHOLOBAH ATAKIWA BAYERN
KLABU ya Bayern Munich inamfuatilia mlinzi wa Chelsea, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 24, huku beki huyo wa kati wa zamani wa kikosi cha England cha vijana wenye umri chini ya miaka 21, akiwa si sehemu ya mipango ya Mauricio Pochettino. **(Mirror)**

### GUEHI KUPIGWA BEI
KLABU ya Crystal Palace itakubali dau la pauni milioni 60 kutoka kwa Manchester United kumnunua beki wa kati wa England, Marc Guehi. **(Teamtalk)**

### MIRANDA ATAJWA NEWCASTLE
NEWCASTLE United iko tayari kuanza mchakato wa ombi jingine la kumnunua mlinzi wa Real Betis, Juan Miranda huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, akitarajiwa kuhamia Ligi Kuu England Januari. **(Fichajes)**

### MUSIALA LULU LIVERPOOL
LIVERPOOL inaaminika kufikiria uwezekano wa kumnunua kiungo nyota wa Bayern Munich, Mjerumani Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 20. **(Football Insider)**

### BOEY ANAVUTIWA ARSENAL
MLINZI wa kulia wa Galatasaray, Sacha Boey mwenye umri wa miaka 23, bado anavutiwa na Arsenal. **(Fotospor)**

### SOLER ANUKIA VILLA
ASTON Villa imeripotiwa kuvutiwa na kiungo wa kati wa Paris St-Germain, Carlos Soler mwenye umri wa miaka 26, kabla ya dirisha la Januari. **(Le Parisien, via Birmingham Mail)**

### LINGARD SAFI SAUDIA
KLABU ya Al-Ettifaq ya Saudi Arabia imeripotiwa kuwa tayari kumpa mkataba mchezaji wa zamani wa Manchester United na England, Jesse Lingard kuelekea dirisha la Januari. **(Goal)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RICE AFUNGUKA KUJIVUNIA UPAMBANAJI WA ARSENAL

**Chelsea walifanya jambo gumu, lakini tulionesha njaa na morali ya kusema haijafika mwisho hadi ifike...**

**LONDON, England**

NYOTA wa Arsenal, Declan Rice, amesema anajivunia morali na upambanaji wa kikosi hicho baada ya kutoka nyuma kwa mabao 2-0 na kupata sare ya 2-2 dhidi ya Chelsea kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumamosi.

Cole Palmer aliwaweka mbele 'The Blues' kwa mkwaju wa penalti, huku shuti kali la Mykhailo Mudryk likiifanya Chelsea kuwa na uongozi wa mabao 2-0.

Rice aliirudisha mchezoni Arsenal baada ya kutumia pasi ya makosa ya golikipa wa Chelsea, Robert Sanchez, kwa kufunga bao kwa shuti kali, kabla ya Leandro Trossard kuisawazishia dakika ya 84.

Baada ya mechi hiyo, Rice aliwasifu wachezaji wenzake kwa pambano lao la kupata pointi dakika za mwisho kwenye Uwanja wa Stamford Bridge.

Akizungumza na Sky Sports, alisema: "Kipindi cha kwanza kutoka kwetu kilikuwa ni kibaya zaidi ambacho tumecheza msimu huu katika suala la uzembe. Lakini sifa kubwa kwa Chelsea, kocha wetu alisema hawakuwa na bahati msimu huu na walifanya iwe ngumu kwetu.

"Ili kuonesha moyo na morali, si rahisi wakati upo nyuma kwa mabao 2-0. Ni juu ya kuwa na vita na mawazo, kusukuma timu na kuhakikisha kila mtu ana imani. Ilikuwa kurudi vizuri.

"Chelsea walifanya jambo gumu, lakini sisi kwenye mpira hatukuwa wazuri vya kutosha - pasi yangu ya kwanza niliitoa. Iliwapa moyo Chelsea, lakini kipindi cha pili tulionesha tunachokihusu - njaa na morali ya kusema haijafika mwisho hadi ifike mwisho.

"Tulionesha moyo mkuu na morali."

Arsenal ilirudi kwenye kiwango ikishika nafasi ya pili katika msimamo nyuma ya Manchester City iliyoshinda dhidi ya Brighton, lakini inaongoza kwa pointi moja tu juu ya Tottenham, ambao jana Jumapili walikuwa wanacheza na Fulham.

Kabla ya mechi za jana ni Arsenal na Tottenham ndio timu pekee hazijapoteza mchezo wowote kwenye mechi za Ligi Kuu England msimu huu.

Rice alifunga bao muhimu ili kuamsha urejesho na anadai kumaliza kwake ilikuwa onesho la silika ya haraka.

Alisema: "Badala ya kuona mpira ukija kwangu nililazimika kukunjuka kwa shuti kali.

"Ilikuwa silika ya haraka kuhusu kupasisha mpira kwa mtu au kuuchukua. Nilikuwa nikipiga kelele, lakini bado tulikuwa chini kwa mabao 2-1 na nilitaka tuendelee na kupata jingine. Nina furaha tulifanya hivyo."

# TEN HAG ATOA USHINDI WA UNITED KWA SIR BOBBY

**SOUTH YORKSHIRE, England**

ERIK ten Hag aliweka wazi ushindi wa Manchester United dhidi ya Sheffield United ulikuwa ni kwa ajili ya gwiji wa klabu hiyo, Sir Bobby Charlton, ambaye alifariki dunia mapema kabla ya mchezo huo.

Huku United wakiomboleza kuondokewa na Charlton ambaye alikuwa na umri wa miaka 86, Scott McTominay alifunga bao la kwanza dakika ya 28.

Lakini kiungo huyo aliadhibiwa dakika sita baadaye kwa kuushika mpira ndani ya eneo la hatari, jambo ambalo lilimruhusu Oli McBurnie kusawazisha kwa mkwaju wa penalti.

Hata hivyo, bao la kustaajabisha la Diogo Dalot liliwahakikishia wageni pointi zote tatu - na Ten Hag alikuwa mwepesi wa kutoa pongezi kwa mshindi wa Kombe la Dunia, Charlton.

Alisema: "Mawazo yetu yako kwa familia yake, haswa mke wake, watoto wake na wajukuu.

"Alichofanikisha katika soka kilikuwa kikubwa sana. Pia haiba yake nje ya uwanja. Ulimwengu wa soka umempoteza mtu mkubwa.

"Tulilazimika kuonesha heshima yetu kwake na nadhani tulifanya hivyo. Tulitaka kusherehekea lakini pia kumkumbuka."



Ushindi wa mfululizo umesaidia kuimarisha meli baada ya United kustahimili mwanzo mbaya wa msimu.

Na Ten Hag alifurahishwa na jinsi timu yake ilivyozoea mbinu zilizotumiwa na bosi wa Blades, Paul Heckingbottom.

Akizungumzia ushindi wa 2-1, alisema: "Tuna furaha na ushindi. Tafuta njia ya kushinda - hiyo ilikuwa mbinu ya mchezo huu.

"Kipindi cha kwanza hakikuwa bora kutoka kwa upande wetu, lakini kutoka kipindi cha pili tulidhibiti mchezo na kushinda kwa bao zuri.

"Sheffield United walikuwa na nguvu nyingi na walicheza kwa mfumo ambao hatukutarajia. Tulijirekebisha baadae."

# Vinicius Junior aisifu Sevilla kufukuza mashabiki wabaguzi

**SEVILLE, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Vinicius Jr, ameipongeza Sevilla kwa kuchukua hatua haraka kumtoa na kumripoti shabiki wake kwa mamlaka kwa madai ya kumtusi kwa rangi yake.

Picha iliyotumwa na Vinicius kwenye mitandao ya kijamii ilionekana kumuonesha mwanamume mmoja akimfanyia ishara ya kibaguzi Vinicius.

Vinicius alisema video ya pili iliyotumwa kwake ilionesha shabiki mwingine mchanga akimtukana.

Baada ya mechi hiyo ya LaLiga, Sevilla ilitoa taarifa kwamba, "mtu mmoja alitambuliwa, alitolewa nje ya uwanja na kukabidhiwa kwa mamlaka ya kisheria".

"Zaidi ya hayo, kanuni za ndani za nidhamu zitatumika kwake na atafukuzwa uanachama mara moja," klabu hiyo ilisema.

Katika taarifa yake, klabu hiyo ya soka iliendelea kusema, "tunalaani tabia yoyote ya ubaguzi wa rangi na chuki dhidi ya wageni, tutaonesha ushirikiano na mamlaka katika kutokomeza tabia hizi, ambazo haziwakilishi mashabiki."

Real Madrid, ambao kwa sasa ndio vinara wa LaLiga walitoka sare ya 1-1 ugenini kwa Sevilla kwenye Uwanja wa Ramon Sanchez-Pizjuan Jumamosi jioni.




Kupitia ukurasa wake wa X, ambayo zamani ilijulikana kama Twitter, baada ya mechi, Vinicius alisema tukio la hivi punde lilikuwa "namba 19 na kuhesabika".

"Hongera Sevilla kwa nafasi yao ya haraka na adhabu katika kipindi kingine cha kusikitisha kwa soka la Hispania, " aliandika.

"Kwa bahati mbaya, nilipata video ya kitendo kingine cha ubaguzi wa rangi kwenye mechi ya Jumamosi hii, safari hii kilifanywa na mtoto.

"Samahani sana hakuna wa kukuelimisha, ninawekeza, na ninawekeza sana katika elimu ya Brazil ili kutengeneza wananchi wenye mitazamo tofauti na hawa.

"Uso wa mbaguzi wa rangi leo umebandikwa kwenye tovuti kama katika matukio mengine mengi. Natumaini mamlaka ya Hispania itafanya sehemu yao na kubadilisha sheria mara moja na kwa wote."

Pia alitoa wito kwa watu waliokamatwa "waadhibiwe kwa jinai" pia.

Vinicius amekuwa akilengwa mara kwa mara na matusi ya kibaguzi kutoka kwa mashabiki wa upinzani.

Mapema mwezi huu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, alitoa ushahidi katika kesi ya mashabiki watatu wa Valencia wanaodaiwa kumuonesha ishara za ubaguzi wa rangi wakati wa mchezo wa Mei katika uwanja wa Mestalla.

# Klopp akiri Konate kustahili kadi nyekundu

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amekiri kwamba beki wake wa kati, Ibrahima Konate, alikuwa na bahati ya kuepuka kadi nyekundu katika ushindi wa mabao 2-0 wa Liverpool dhidi ya Everton, Jumamosi.

Beki wa pembeni wa Everton, Ashley Young, alitolewa mwisho wa kipindi cha kwanza baada ya kupata kadi mbili za njano kwa kumchezea vibaya Luis Diaz.

Konate, ambaye tayari alikuwa na kadi ya njano, alimchezea faulo Beto na kumdondosha chini, lakini akaepuka kadi ya pili, huku mwamuzi Craig Pawson akitoa ya onyo kwa bosi wa Everton Sean Dyche kwa malalamiko.

Klopp alijibu tukio hilo kwa kumtoa Konate mara moja, na alikiri baada ya mchezo huo kuwa Mfaransa huyo alikuwa na bahati ya kubakia uwanjani.

"Ibrahima, angeweza kuondoka, ndio," bosi wa Liverpool aliiambia BBC Sport. Ingeweza kutokea kwa uwazi, tukawahi kumtoa na kutoka wakati huo tulikuwa imara na tulivu."

Klopp alifurahishwa na jinsi timu yake ilivyocheza, na kuongeza: "Niliipenda sana. Ni dabi unapaswa kuzingatia mambo tofauti kwa pasi bora ya mwisho katika kipindi cha kwanza wakati tukiwa mbele kwa mabao 3-0.

"Hatukuruhusu kufanya walivyotaka. Tulikuwa wazi katika changamoto. Ni ngumu kwa sababu ilikuwa kizuizi kirefu na walibadilika kidogo na kuweka kwa nguvu zetu.

"Nilipenda muda mwingi na kadi nyekundu ilikuwa na ushawishi mkubwa kwenye mchezo. Nilitaka tuwe watulivu na tupuuze kuwa sisi ni mtu mmoja. Ni ngumu kwenye majukwaa kwa sababu ni kama sasa unapaswa kuunda na kila mmoja. kumiliki mpira na ilichukua muda hadi tukapata nafasi. Na kisha penalti. Niliiona ni penalti ya wazi."



HABARI MICHEZO

# BALEKE FUNDI KINARA WA MGUU WA KULIA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

HUKU akiwa amekaa kileleni mwa orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu Bara baada ya kucheka na nyavu mara tano hadi sasa msimu huu, Straika wa Simba, Jean Baleke, mabao yake yote matano amefunga kwa mguu wa kulia.

Kwa mujibu wa takwimu zetu, Baleke raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, anafuatiwa na Matheo Antony, straika wa Mtibwa anayeshika nafasi ya pili kwa kufunga mabao kutumia mguu wa kulia, akiwa amefanya hivyo mara tatu na ana idadi hiyo ya mabao.

Wachezaji wanaokamata nafasi ya tatu kwa kupachika mabao kwa mguu wa kulia ni wale waliopachika mabao mawili mpaka sasa.

Nao ni Prince Dube na Feisal Salim wote wa Azam FC, Stephane Aziz Ki, Mudathir Yahaya na Maxi Nzengeli na Pacome Zouzoua wote wa Yanga, Eric Okutu wa Tabora United na Saido Ntibazonkiza wa Simba.


Wakati huo huo, mchezaji Yassin Mgaza wa Dodoma Jiji anaongoza kwa kufunga bao la mapema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

Amefanya hivyo dakika ya kwanza ya mchezo dhidi ya Tabora United Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi Oktoba 6, mwaka huu timu yake ikipoteza kwa mabao 2-1.

Yanafuatiwa na mabao yaliyofungwa dakika ya tatu na Zouzoua wa Yanga katika mechi dhidi ya Ihefu, ikishinda mabao 3-0 na Feisal Salum wa Azam FC kwenye mchezo ambao walicheza dhidi ya Tabora United kwa na kushinda mabao 5-0.

Mabao mengine yaliyotinga dakika ya tano ambayo yalifungwa na Prince Dube wa Azam FC kwenye mechi dhidi ya Tabora United, Elius Maguri wa Geita Gold alifunga dhidi ya Ihefu na Baleke akifunga dhidi ya Mtibwa Sugar.

## HISTORIA IMEANDIKWA...



Rais wa Heshima na Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Mohamed 'Mo' Dewji (katikati), akipozi katika picha ya pamoja na Rais wa FIFA, Gianni Infantino (kushoto) na Rais wa CAF, Patrice Motsepe, wakati wa mechi ya ufunguzi ya African Football League kati ya Simba na Al Ahly ya Misri iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Ijumaa iliyopita na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2. **MPIGAPICHA WETU**

# Basena aahidi mazuri zaidi Ihefu

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mganda, Moses Basena juzi alianza kibarua chake cha kuinoa Ihefu FC kwa suluhu ya bila kufungana nyumbani katika Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya dhidi ya Coastal Union.

Ilikuwa pia ni sare ya kwanza kwa Ihefu msimu huu, kwani ilicheza mechi tano ikishinda mbili na kupoteza tatu, kabla ya suluhu hiyo kwenye raundi ya sita ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Basena, kocha wa zamani wa Simba, amechukua nafasi iliyoachwa wazi na Zuberi Katwila ambaye inasemekana huenda akatua Mtibwa Sugar.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, kocha huyo alisema kuna mapungufu fulani ambayo ameyaona na atayafanyia kazi.

"Malengo ya mechi tumefanikiwa kwa asilimia 50, kwa sababu hatujaruhusu bao na tumekosa nafasi nyingi za kufunga, vijana hawajacheza vibaya sana, ila kuna mapungufu kidogo, kukimbia kwenye nafasi ambazo wanaweza kuwa hatari kwenye lango la mpinzani ndicho kinachosumbua, niitaanza kulifanyia kazi na mashabiki wa Ihefu watarajie mazuri," alisema kocha huyo aliyewahi pia kuwa kwenye jopo wa makocha wa Timu za Taifa za Uganda na Tanzania kwa nyakati tofauti.

Ihefu imefikisha pointi saba na baada ya mechi hiyo ilikwea hadi nafasi ya tisa ya msimamo.

Hali ni mbaya kwa Coastal Union ambayo haijashinda hata mechi moja mpaka sasa ikiwa kwenye nafasi ya 15 ya msimamo na pointi zake tatu.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Fikirini Elius, alisema wanashukuru kupata hata hiyo pointi moja.

"Tulikuwa na malengo mawili katika mechi ya leo, kwanza ni kutafuta ushindi, lakini hata kama tukikosa tupate walau pointi moja kwa sababu tulikuwa tunacheza ugenini na Ihefu ni timu nzuri, na ndiyo maana muda ulivyozidi kwenda tulikuwa tukizuia zaidi, naamini baadaye timu itakaa vizuri.

## Yanga, Azam ni vita ya kileleni

INATOKA UK. 24

wanavyocheza utakuwa mchezo wa mbinu na ufundi zaidi," alisema Gamondi.

Mwakilishi wa wachezaji wa Yanga, Mahletse Makudubela 'Skudu', alisema mechi itakuwa ya ushindani mkubwa, ila watatumia akili na nguvu kuhakikisha wanavuna alama tatu muhimu dhidi ya Azam FC.

"Kikubwa alama tatu hatuangalii mchezaji anacheza kwa kiwango kipi kikubwa ni kupambana kuhakikusha tunapata alama muhimu ili kujiweka katika nafasi nzuri katika mbio zetu za ubingwa," alisema Skudu.

Kocha wa Azam FC, Bruno Ferry, alisema wamejipanga vizuri na kwamba kikosi chao kipo tayari kwa ajili ya kutafuta alama muhimu, lakini akikiri hajui nini kitatokea ila wanaenda kupambania matokeo chanya.

"Utakuwa mchezo wa kimbinu na kiufundi, tulipoteza mechi ya Ngao ya Jamii, hatutakuwa tayari kupoteza mechi kwa mara ya pili, tumejipanga vizuri kuhakikisha tunapata matokeo chanya,"alisema Ferry.

## Simba: Al Ahly hawataamini

INATOKA UK. 24

mechi itakuwa ngumu, lakini tunajiamini, kwa namna tulivyowaona Al Ahly, naamini Simba tuna uwezo mkubwa wa kupambana nao kwa dakika 90 zingine na kuwang'oa.

Ukiuangalia ule mchezo utagundua kuwa Simba tumegharamika na makosa yetu sisi wenyewe, lakini si ubora wa wapinzani wetu, najua kwa sasa mwalimu wetu ana kazi kubwa ya kuyaondoa makosa yanayotugharimu kwenye mazoezi ili Al Ahly wasinufaike nayo kwa mara nyingine tena," alisema Meneja Habari huyo.

Aliwataka wanachama na mashabikiwa Simba wasiwe na wasiwasi badala yake kuiombea ili kuweza kuing'oa Al Ahly.

"Niwaambie tu wanachama na mashabiki wa Simba hawapaswi kuwa na hofu, hii siyo timu ya kutufanya tuwe na wasiwasi sana, si kama hawawezi kutufunga au si timu kubwa, hapana ni Mabingwa wa Afrika na wanauwezo mkubwa sana, ila hawana uwezo wa kutufunga kwa kutudhalilisha, au kututawala.

"Wachezaji wetu wakiamua kupambana chochote kinaweza kutokea, kumbuka baada ya kutufunga mabao 5-0, mwaka 2019 ilikuwa ndiyo mwisho wa wao kutudhalilisha, matokeo yake sasa ikawa inatufunga bao moja tu kwao, na hiyo ilikuwa timu iliyopita, safari hii tutawashangaza," alisema.

# Michezo

Jumatatu Oktoba 23, 2023

Nipashe




%%%%%%


**Rice afunguka kujivunia upambanaji wa Arsenal** UKURASA 21


**TUPO TAYARI...**



Wachezaji wa Simba wakiwasili jijini Cairo, Misri jana mchana tayari kwa mchezo wa marudiano wa robo fainali ya African Football League dhidi ya Al Ahly ya nchini humo utakaopigwa kesho. Mechi ya kwanza katika Uwanja wa Benjamin Mkapa wiki iliyopita ilimalizika kwa sare ya mabao 2-2. **PICHA: SIMBA**

# YANGA, AZAM FC NI VITA YA KILELENI LIGI KUU LEO

## ●●●Makocha wote wafunguka huku kila mmoja akiweka matumaini ya ushindi, lakini...

**Na Saada Akida**

LEO mtoto hatumwi dukani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam wakati Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga watakapovaana na Azam FC.

Mchezo huo unasubiriwa kwa hamu na wadau wa soka kutokana na timu hizo zinapokutana kuonesha ushindani mkubwa kwa kila moja kuhitaji alama muhimu.

Timu hizo zinakutana leo kwa mara ya pili kwa msimu huu baada ya awali kuvaana kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii ambapo Azam FC ilikubali kichapo cha mabao 2-0 katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Katika mchezo huo, Yanga ni wenyeji wakiwa kwenye nafasi ya tatu kwa alama 12 na Azam FC pointi 13 wakiwa nafasi ya pili nyuma ya vinara wa ligi hiyo, Simba walioshinda mechi zao zote tano kwa asilimia 100.

Kuelekea mechi hiyo ya leo, Yanga ni bora katika safu ya ushambuliaji ikiongoza kwa kufunga mabao 15 ikiruhusu kufungwa mawili sawa na Azam FC ambayo hadi sasa msimu huu ina mabao 10 ya kufunga, hiyo ikionesha katika safu ya ulinzi timu zote zipo vizuri.

Ni mchezo wenye presha kwa timu zote kwa sababu Yanga itataka kushinda ili kulinda taji lakini pia Azam FC nao wanahitaji alama tatu ili kuendelea kuwapo juu kwenye mbio za ubingwa, kwani kama itafanikiwa kuvuna alama zote tatu itakaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kwa alama 16 na kuishusha Simba ambayo haitakuwa na mchezo wa ligi hiyo kwa sababu ya ushiriki wao wa michuano ya Afrika Football League, AFL.

Lakini pia kama Yanga ikishinda itafikisha alama 15 sawa na Simba itakayokuwa na mchezo mmoja mkononi, na inaweza kuwashusha Wekundu wa Msimbazi hao kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa kutokana na vinara wa ligi hiyo kucheka na nyavu mara 14 na kuruhusu manne hadi sasa.

Makocha wa timu hizo wakizungumzia mchezo huo, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi alisema wamefanya maandalizi mazuri ya kucheza na Azam FC kama wanavyocheza na timu yeyote na kikubwa anahitaji alama tatu ili kufikia malengo yao.

Alisema Azam FC ni timu nzuri na ina wachezaji wazuri, ila wanafurahi kurejea Uwanja wa Mkapa ambao wanaamini watatenda kupata matokeo chanya kwa kuibuka na alama tatu ili kujiweka kwenye nafasi nzuri kwenye mbio zao za ubingwa.

"Tutamkosa Farid Mussa aliyekuwa majeruhi na sasa amerejea kwenye mazoezi, tumejiandaa vizuri kikosi kipo sawa kwa ajili ya mchezo kutafuta alama tatu muhimu.

"Azam FC ni timu nzuri, ila nimefanikiwa kuwasoma wapinzani wetu hao, tunajua


INAENDELEA UK. 23


## Simba: Al Ahly hawataamini

**Na Adam Fungamwango**

TAYARI Kikosi cha Simba cha wachezaji 24 kimetua jijini Cairo, Misri kwa mkwara mkubwa, huku Kocha Mkuu wa timu hiyo, Roberto Oliveira na Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, wakisema wana kazi moja tu ya kuwashangaza Wamisri nyumbani kwao hapo kesho watakapocheza mechi ya marudiano dhidi ya Al Ahly.

Simba ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Mafarao hao katika mechi ya ufunguzi wa michuano ya African Footbal League (AFL), iliyochezwa Ijumaa iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Robertinho alisema wanakwenda kucheza mechi ngumu dhidi ya Mabingwa wa Afrika, lakini ana imani na wachezaji wake watafanya kile ambacho amewatuma, nacho ni kupambana, kutumia vipaji walivyonavyo, kufuata maelekezo yake na kucheza kwa kujiamini.

"Wapinzani wetu ni timu ngumu, inawezekana ikawa ndiyo timu bora Afrika, lakini angalia tulicheza vizuri sana hasa kipindi cha pili, kocha unapofanya mabadiliko ya kuwaingiza wachezaji unatarajia wakafanye mabadiliko ya kweli, na uliona mfano alipoingia Sadio Kanoute, Jean Baleke, Israel Mwenda mpira ulibadilika na hiyo ilinifurahisha sana, msimu uliopita haikuwa hivyo, ukipanga kikosi cha kwanza bado hicho hicho ndiyo bora, hata ukiingiza wachezaji wa akiba hawaendi kubadisha chochote. Bado mpaka sasa naangalia ni mfumo gani tutautumia kwenye mechi hii ya marudiano," alisema kocha huyo.

Naye Ahmed alisema mipango ya kuing'oa Al Ahly ipo pale pale, japo ilishindikana Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Tunataka kutimiza mipango yetu, nayo ni ile ile ya kuitoa Al Ahly, tumeshindwa kumfunga nyumbani baada ya matokeo ya sare ya mabao 2-2, sasa kazi hii tunataka tuifanye kwao, tunajua


INAENDELEA UK. 23



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >